SUPA JACKPOT
TZS. 1,072,549,524
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#



UKURASA 3

**Wafanyakazi** Elimu ya Juu waliibua tena sakata la kikokotoo cha mafao




UKURASA 9

Nipashe
MWANGA WA JAMII
JUMAPILI
Jumapili Februari 5, 2023 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
www.ippmedia.com
ISSN 0856 • No. 0581212
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US



# Lissu afichua siri alivyopigwa risasi

**•Amtaja** Mungu kumtumia dada wa kazi kumnusuru... *Endelea Ukurasa.8*

## YALIYOMO

UKURASA WA 4 & 5

### SURA YA CCM MPYA CHINI YA RAIS SAMIA



LEO Chama Cha Mapinduzi (CCM) kinaadhimisha siku ya kuzaliwa, ikitimiza umri miaka 46. Si haba, sura ya nusu karne na waliozaliwa zama hizo, umri wao sasa wako njia panda kuelekea kwenye...

UKURASA WA 17

### VIONGOZI EAC WAJADILI MAPIGANO DRC

VIONGOZI wa mataifa ya Jumuiya ya Afrika Mashariki wanakutana nchini Burundi, kujadili mapigano yanayoendelea mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasi...

## CCM yalia na michezo ya kubahatisha

UKURASA 3



Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla (kushoto), akiwajulia hali majeruhi wa ajali ya Mitsubishi Fuso na Toyota Coaster iliyokuwa imebeba mwili wa marehemu iliyotokea eneo la Magila Gereza, Korogwe, Barabara Kuu ya Segera Buiko, waliolazwa katika Hospitali ya Rufani ya Bombo mkoani Tanga, jana. Watu 17 walifariki dunia na wengine kujeruhiwa. Picha ndogo: mabaki ya Coaster. **PICHA: OSCAR ASSENGA**

# Ajali ilivyowaua 17 wakisafirisha maiti

UKURASA 2

MICHEZO YANGA YAIWAZA ROBO FAINALI CAF UK. 24 MAONI, KATUNI UK.6

# Ajali ilivyowaua 17 wakisafirisha maiti

Na Waandishi Wetu


Mmoja wa majeruhi wa ajali hiyo akipokelewa katika Hospitali ya Mkoa wa Tanga, Bombo. **PICHA: OSCAR ASSENGA**

WATU 17 wamefariki dunia na majeruhi 12 katika ajali iliyohusisha Mitsubishi Fuso na basi dogo aina ya Toyota Coaster lililokuwa limebeba mwili wa Athanas Mrema likienda Rombo, Kilimanjaro kwa ajili ya mazishi baada ya kugongana uso kwa uso.

Ajali hiyo ilitokea juzi majira ya saa 4.30 usiku eneo la Magila Gereza, Mombo Wilayani Korogwe, barabara Kuu ya Segera - Buiko mkoni Tanga.

Katika ajali hiyo, sanduku lililokuwa limebeba mwili wa marehemu lilivunjika na kubaki vipande vipande, hivyo mwili kupelekwa chumba cha maiti katika Hospitali ya Wilaya ya Korogwe kuhifadhiwa.

Waliofariki dunia katika ajali hiyo ni ndugu 14 wa familia moja wakiwemo watoto wa marehemu, baba mkubwa, dada na baba mdogo.

Ndugu hao ni Lizybetha Lamesay, Elizabeth Mrema, Godwin Mrema, Kennedy Mrema, Athanas Mrema, Avelina Mrema, Emilian Lyakurwa, Agustina Mrema, Nestom Kiwango, Rozina Lamosai, Suzana Mrema, Julietha Mrema na Ethan Peter.

**SAMIA AWALILIA**

Kutokana na ajali hiyo, Rais Samia Suluhu Hassan amesema amesikitishwa na vifo vya watu hao.

"Nawapa pole wafiwa wote walioguswa na vifo hivi. Nawaombea ndugu zetu hawa wapumzike mahali pema na majeruhi wapone," ulisomeka ujumbe wa Rais Samia katika mtandao wa kijamii wa Twitter.

Aidha, Chama cha Wananchi (CUF), kililelezea kupokea kwa huzuni na masikitiko taarifa ya vifo hivyo.

"Chama kinatoa pole kwa wafiwa wote na kuwaombea majeruhi wapone haraka ili waendelee na majukumu yao ya kila siku. Lakini chama kinatoa wito kwa madereva na watumiaji wengine wa barabara kuzingatia sheria na matumizi sahihi ya barabara ili kupunguza ajali na maafa yatokanayo na ajali hizo," ilisema taarifa hiyo ya CUF.

Awali, akizungumza na waandishi wa habari, Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Omary Mgumba, alisema amepokea kwa masikitiko tukio la ajali mbaya iliyotokea usiku wa kuamkia jana na kusababisha uharibifu mkubwa wa magari hayo.

Mgumba alisema gari lenye usajili namba T.673 CUC, Mitsubish Fuso likiendeshwa na dereva ambaye jina lake halijafamika, liligongana na gari T.863 DXN Coaster iliyokuwa imebeba mwili wa marehemu na wanafamilia.

Alisema katika Coaster hiyo kulikuwa na abiria 26 waliotoka Dar es Salaam kwenda Rombo kwa mazishi ya ndugu yao.

Pia alisema miili ya marehemu imehifadhiwa katika Hospitali ya Wilaya ya Korogwe, majeruhi 10 wamehamishiwa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Tanga ya Bombo na wengine wawili wamebaki Korogwe.

Alisema chanzo cha ajali ni mwendokasi na uzembe wa dereva wa Mitsubishi Fuso aliyekuwa akijaribu kulipita gari la mbele bila kuchukua tahadhari, hivyo kugongana uso kwa uso na Coaster.

Baada ya kukaguliwa kwa ajali hiyo, Mgumba alisema magari hayo yameshaondolewa barabarani ili kuruhusu barabara kupitika.

**MAJERUHI HALI MBAYA**

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Tanga ya Bombo, Dk. Naima Yusuph, alithibitisha kupokea majeruhi 12 jana majira ya saa 11:30 alifajiri na wanaendelea na matibabu chini ya uangalizi wa madaktari wakisubiri ripoti ya daktari aliyewafanyia uchunguzi wa kina.

"Isipokuwa watano hali zao si nzuri na wawili inawezekana wakapatiwa rufani kwenda Hospitali ya Taifa ya Muhimbili," alisema Dk Yusuph huku akibainisha kuwa majeruhi hao walipokewa wakiwa na majeraha makubwa, hivyo kulazimika kupelekwa kwenye chumba cha uangalizi maalumu.

**HEMED ATEMBELEA MAJERUHI**

Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, aliwatembelea majeruhi hospitalini hapo na kuwapa pole. Kiongozi huyo aliambatana na Mgumba, Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Tanga, Rajab Abdallah na viongozi viongozi wengine wa chama na serikali mkoani Tanga.

**MASHUHUDA WASIMULIA**

Shuhuda wa ajali hiyo, Gines Mrema, alisema marehemu Mrema (waliyekuwa wakienda kumzika) ni baba yake mdogo, alisema ndugu yao alikuwa anaishi Mbezi kwa Msuguri, alianza kuumwa na kufikishwa katika Hospitali ya Bochi kabla ya kufariki dunia.

Alisema juzi waliendа kuchukua mwili huo kwa ajili ya kuusafirisha kwenda Rombo Mkuu na wakiwa katika gari lililokuwa na wanafamilia wengi, walipata ajali ya kugongana uso kwa uso na Fuso eneo la Korogwe.

"Wamefariki (dunia) ndugu zetu 14 na wale wa fuso walikuwa watatu ukijumlisha na wa kwetu tunafikia idadi ya 17," alisema.

Alibainisha kuwa katika ajali hiyo wamo watoto wawili wa marehemu wawili na upande wa baba yake wamefariki dunia dada yake aliyekuwa na watoto, baba mdogo na ndugu wengine.

Manusura mwingine wa ajali ambaye amelazwa Bombo, Erick Edward Mrema, akizungumza namna ajali hiyo ilivyotokea, alisema wakati wanasafirisha mwili wa ndugu yao kwenda kuzika, walipofika eneo la Korogwe walikumbana na mkasa huo mzito.

Alisema lilitokea lori na kuigonga Coaster waliyokuwa wamepanda na kuwapoteza ndugu zao 14 akiwamo dada yake aliyekuwa na mtoto.

Erick alisema kabla ya ajali hiyo, walikuwa na safari nzuri huku akisema katika safari hiyo, yeye alikaa nyuma pamoja na mtoto wake na anamshukuru Mungu wamenusurika.

**WAFIKA KUTAMBUA NDUGU**

Ridhiwani Mbwambo ambaye ni mkazi wa Kijiji cha Kileo, Mwanga Mkoani Kilimanjaro alilazimika kufunga safari kufika Jijini Tanga kutafuta ndugu zake wawili na tayari amempata mmoja.

Alisema baada ya kusikia taarifa za ajali hiyo, aliamua kufunga safari kukimbilia Hospitali ya Magunga, Korogwe kusaka ndugu zake na alipowakosa akaenda Bombo.

Daktari wa Dharura Bombo, Dk. Arafa Abubakar, alisema majeruhi waliopokewa wanaendelea vizuri isipokuwa wawili waliumia vibaya kichwani na watapewa rufani kwenda Muhimbili.

**KUZIKWA JUMATATU**

Msemaji wa familia na kaka mkubwa wa marehemu Atanas Mrema (59), Colman Mrema, alisema wamepata msiba mzito na baada ya kikao wamekubaliana kuzika Jumatatu kwa baadhi ya wanafamilia.

Alisema marehemu Mrema alikuwa na watoto sita, wa kiume wakiwa watano, wa kike mmoja, ambaye amefariki dunia katika ajali hiyo.

Aliishukuru serikali ya wilaya ambayo alisema imeahidi kuwapatia usafiri wa kufikisha miili yote katika maeneo ambayo watafanya mazishi.

***Imeandikwa na Oscar Assenga (Tanga), Mary Mosha (Rombo), Godfrey Mushi (Arusha) na Beatrice Shayo (Dar).**

**HABARI KITAIFA**

# CCM yalia vijana kutekwa na michezo ya kubahatisha

**Na Mary Geofrey,** MOROGORO

KATIBU Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Daniel Chongolo amewataka vijana nchini kuacha kubahatisha maisha kwenye vibanda vya kamari.

Chongolo alitoa kauli hiyo jana alipozungumza na wanachama wa CCM na wananchi nyumbani kwa mjumbe wa shina namba moja kwenye Kijiji cha Ngerengere wilayani Morogoro katika mwendelezo wa ziara yake mkoani Morogoro.

Alisema ili kufanikisha maisha ni lazima uwe na bidii kazini na kujituma ili kufikia malengo na ndoto badala ya kukaa vijiweni.

"Ukikutana na vijana waliopo kwenye bao, ndio mabingwa wa kuongea uongo na wepesi wa kudanganywa kirahisi. Anaambiwa wewe cheza bao jioni kuna mkeka (orodha ya mechi alizoweka fedha ili shinde dau kubwa)," alisema Chongolo.

Alisema vijana wanajishughulisha na mkeka wa kubahatisha kuanzia asubuhi hadi jioni bila kuingiza chochote kwenye maisha yao.

"Kazi kubwa ni kubeti, beti, beti, unajiuliza wewe kijana mwenye nguvu na rijali kabisa, unakaa kusubiri uandike karatasi, timu fulani na timu fulani itashinda ili uishi! Ninajua kuna watu ninawaharibia biashara lakini lazima tuambiane ukweli," alisema Chongolo.

Alisema lazima vijana waachane na tabia ya kuishi maisha ya kubahatisha, wafanye biashara ambazo zinawapa matokeo mwishoni.

"Achaneni na hii, unatafuta Sh. 20,000 kila siku, kwenda kumpatia mtu huko, yeye anapata kipato wewe unabaki unapata kipato gani?" alihoji Chongolo.

Alisema kuna fursa nyingi zinatokea nchini zinazohitaji vijana wenye ujuzi, ukiwamo Mradi wa Reli ya Kisasa (SGR), ambao umeajiri vijana wenye ujuzi wa kuchomelea chuma na kazi nyingine.

Alisema Vyuo vya Ufundi Stadi (VETA) wanafundisha ufundi wa kuchomea, vijana wengi wanaopata ujuzi hawakosi kazi za kufanya.

"Vijana nendeni mkajifunze ujuzi wa mambo mbalimbali VETA, kwa ajili kuendesha magari makubwa, fursa zipo ukija ujenzi wa barabara na wewe mambo yanakunyookea.

"Mradi wa reli ulikuja hapa, vijana si walipata kazi! waliokosa ni kinanani? si wanaokaa kienyeji si ndio! Kwa hiyo, msikae kienyeji, wapelekeni vijana VETA wakajifunze ujuzi wa mambo mbalimbali," aliagiza.

Pia alisema vijana wengi wanajiingiza kwenye wizi na unyang'anyi wa mali za watu kwa sababu ya kukosa maadili.

Alisema vijana hawataki kujishughulisha, wanataka mali za haraka bila ya kuwa na ujuzi wowote licha ya serikali kuwekeza nguvu kubwa, kujenga vyuo vya ufundi na shule za sekondari ili kupata elimu.

Katibu wa Halmashauri Kuu Itikadi na Uenezi, Sophia Mjema aliwataka wazazi na walezi kuwahimiza vijana kutumia fursa ya vyumba vya maharasa vilivyojengwa nchini kote kwenda kupata elimu kwa ajili ya kujiandalia kesho yao.

# Wafanyakazi waliibua tena sakata la kikokotoo mafao

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

CHAMA cha Wafanyakazi wa Taasisi za Elimu ya Juu Tanzania (THTU) kimewasilisha andiko lenye mambo manane serikalini yanayohusu uchambuzi wa kina wa maslahi ya wafanyakazi kwa ajili ya kutafutiwa ufumbuzi, ikiwamo kuendelea kuboresha kikokotoo cha mafao ya kustaafu kwa njia za utafiti na majadiliano.

Mwaka jana serikali ilitangaza kikokotoo kipya cha mafao ya mkupuo kuwa ni asilimia 33.

Akizungumza juzi wakati wa uapisho wa viongozi wa taifa wa THTU, Mwenyekiti wa THTU Taifa, Dk. Paul Loisulie alisema katika andiko hilo, wamechambua kwa kina masuala hayo na kuonyesha chanzo chake, madhara, namna ya kutatua na tija itakayopatikana baada ya kutatuliwa.

Alitaja masuala mengine waliyowasilisha serikalini kuwa ni malalamiko juu ya marekebisho ya Sheria ya Utumishi wa Umma kuhusu muda wa kustaafu watumishi na wanataaluma.

"Malalamiko yaliyojitokeza kwa watumishi wa umma yanayolenga Waraka wa Msajili wa Hazina Na. 6 wa Mwaka 2015 ambao unaleta athari kubwa kwa mishahara ya wafanyakazi waendeshaji wa mkondo wa PGSS," alisema.

Pia alisema wamegusa kukosekana kwa sheria ya kazi na miongozo ya serikali inayoweka viwango vya mishahara katika sekta binafsi na taasisi za elimu ya juu.

"Masuala yaliyobakia kupatiwa ufumbuzi katika Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) likiwamo suala la ushirikishaji wa vyama vya wafanyakazi kwenye Bodi ya HESLB na mengine machache, ucheleweshwaji wa mafao kwa wastaafu, kukosekana kwa fao la huduma ya afya baada ya kustaafu, kusitishwa kwa nyongeza ya mwaka ya mshahara kwa watumishi," aliyataja.

Alieleza mabadiliko ya sheria ya utumishi wa umma ambayo yanaleta athari kwa taratibu za nidhamu kwa watumishi wa umma kutokana na kile alichokiita matumizi mabaya.

Kuhusu masuala ya utafiti, Dk. Loisulie alishauri kuwe na mfumo wa kuzipata taarifa zote za utafiti unaofanyika nchini, kuwe na sera na mwongozo unaowataka watafiti kuhakikisha kuwa matokeo ya utafiti yanarejeshwa kwenye jamii ili yatumike na kuleta tija katika maendeleo ya nchi.

"THTU inapendekeza kuwapo kwa mkakati wa wazi wa kuwashirikisha watunga sera na utafiti ili kuhakikisha kwamba utafiti unakuwa na majibu ya hoja zilizopo kwenye vipaumbele vya utafiti vya taifa, utafiti usiachwe katika makabati na maktaba bila kujulikana kwa walengwa wa utekelezaji wake, kuongeza kiwango cha fedha ambazo zinatengwa kutoka kwenye pato la taifa ili ziende kwenye utafiti," aliwasilisha hoja yao.

Pia alisema taasisi za elimu ya juu zitakiwe kutenga kiasi fulani cha bajeti kwa ajili ya kufadhili utafiti wenye mwelekeo wa maendeleo ya taifa.

Akizungumza kwenye hafla hiyo, Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Patrobas Katambi aliahidi yale yote waliyoandika, atakwenda kufanyia kazi yaliyopo kwenye ofisi yake na yale ya Ofisi ya Rais atayafikisha sehemu husika.

"Suala la kikokotoo, nimpongeze Rais, mnyonge mnyongeni lakini haki yake mpeni, tumetoka asilimia 25, ninakumbuka ilikuwa jasho kweli, vilikuwa vikao vingi na TUCTA (Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi), angalau kikae sawa.

"Rais kwa mapenzi yake na kutokana na kupokea nchi ikiwa kwenye changamoto nyingi, mapokeo ya hali ya uchumi, hata kwenye familia zetu tunajua changamoto za corona, bado akasema hapa tutatoka asilimia 25 twende 33, ndio alikuwa ameanza hata mwaka mmoja hajamaliza, anastahili pongezi," alisema.



Ofisa Elimu Msingi wa Manispaa ya Temeke, Abdul Buhety (kushoto), akikabidhi zawadi ya kompyuta mpakato kwa Mwanafunzi Bora wa Shule ya Sekondari ya Al- Hikma, Abdulkarim Ahmed, aliyepata divisheni 1.7 katika mtihani wa kidato cha nne mwaka jana, katika hafla ya kuwapongeza wanafunzi wa kidato hicho jijini Dar es Salaam jana. Shule hiyo, imeshika nafasi ya pili katika shule za kiislam nchini. Wa (pili kushoto) ni Mkurugenzi wa Taasisi ya Al- Hikma, Nurdin Kishik. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Chongolo acharuka kituo afya kutofanya kazi miaka mitatu

**Na Mary Geofrey,** MOROGORO

KATIBU Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Daniel Chongolo ametoa siku 14 kwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Angellah Kairuki kutembelea Kituo cha Afya Mikese ambacho baadhi ya majengo yake yamekaa zaidi ya miaka mitatu bila kutumika kutokana na kukosa vifaa vya matibabu.

Pia ameonyesha kuchukizwa na tukio hilo lililofanywa na Halmashauri ya Morogoro Vijijini ambayo imeshindwa kutenga fedha kutoka kwenye fedha zake za ndani, kununua vifaa ili huduma kuanza kutolewa kituoni huko ilhali kuna Sh. bilioni 2.5 zilizobaki kwenye bajeti ya fedha za mwaka wa fedha uliopita.

Chongolo alitoa agizo hilo jana wakati akizungumza na wanachama wa CCM na wananchi wa Kijiji cha Mikese wilayani humo baada ya kutembelea kituo hicho na kukuta majengo ya wagonjwa yaliyojengwa mwaka 2019 kwa gharama ya Sh. milioni 560 yakiwa hayatumiki.

"Hatuwezi kwenda namna hii, nitakwenda kuzungumza na Waziri wa TAMISEMI aje mwenyewe hapa ndani ya siku 14, aone fedha zilizowekwa hapa kwa ajili ya kujenga majengo haya lakini hayatumiki, haiwezekani.

"Hata tukiwaleta watumishi wa afya waliopangwa hapa, ninadhani wanatushangaa maana hawana kazi ya kufanya, madaktari nao hawana kazi wanatamani vifaa vingekuwapo wafanye kazi.

"Na sisi tukija hapa tunasema kidumu Chama Cha Mapinduzi, kitadumu kama mambo yatanyooka, hivi hatuwezi kudumu kama wenyewe tunajihujumu. Haiwezekani hata kidogo. Nimechaguliwa kuwa Katibu Mkuu wa chama, nikaona mambo ya ovyo nikapiga makofi hapa, nitakuwa simtendei haki aliyenipa dhamana hii Mwenyekiti wangu wa chama ambaye pia ni Rais wa Tanzania," alisema Chongolo.

Alisema wao wanakagua utekelezaji wa ilani ya uchaguzi na kama mambo hayaendi vizuri, watachukua hatua.

"Hili halikubaliki tukiona mambo hayaendi tutachukua hatua zaidi," alionya Chongolo.

# INAPOSHEREHEKEA MIAKA 46 KUZALIWA...

# Sura ya CCM mpya chini ya Rais Samia

**Na Mwandishi Wetu**

LEO Chama Cha Mapinduzi (CCM) kinaadhimisha siku ya kuzaliwa, ikitimiza umri miaka 46. Si haba, sura ya nusu karne na waliozaliwa zama hizo, umri wao sasa wako njia panda kuelekea kwenye uzee.

Ni chama kilichoongozwa na wenyeviti sita tangu kuzaliwa kwake na kwa mujibu wa utaratibu wa ndani uliowekwa, ni kwamba kila anayepata nafasi ya Urais, hukasimiwa uenyekiti wa chama.


CCM tangu kuanzishwa, imeendeleza historia ya kubaki chama tawala kitaifa katika Jamhuri ya Muungano Tanzania. Lakini la ziada kwenye hatua iliyofikiwa sasa, kwa mara ya kwanza ina mwenyekiti mwanamke, kama ilivyo nafasi anayoishika mama huyo huyo ya urais.

Hivyo, mara tu baada ya kuapishwa Machi 19, 2021 kuwa Rais baada ya kifo cha mtangulizi wake, Rais Dk. John Magufuli, wiki sita baadaye mwishoni mwa mwezi Aprili mwaka huo, Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) ya CCM, ilimpitisha Dk. Samia kuwa Mwenyekiti wake wa Taifa.

Mara zote katika siasa kuanzia nadharia zilizopo kitaaluma, hadi kwenye uhalisia ulingoni kwa mwanasiasa mmoja mmoja, au chama kwa ujumla, nyenzo muhimu katika kuifanikisha ipige hatua ni umuhimu wa kufanikisha kinachoitwa 'kukubalika' au wenye taaluma hiyo wanaiita 'legitimacy,'

**ANAIENDESHAJE CCM?**

Kama ilivyo misingi ya kikatiba nchini ndani na nje ya chama, asili ya siasa na uongozi kitaifa ambao Rais Dk. Samia amekuwa akiusimamia, unawaegemea 'wakulima na wafanyakazi.'



Mwalimu Julius Nyerere, Mwenyekiti muasisi wa CCM.

Katika zama zake Dk. Samia akiiongoza CCM, naye kama walivyo watangulizi wake, anajikita katika kuhakikisha anashuhudia mamlaka za kiserikali zinatenda zilivyoelekezwa na chama, kuwafikia na kuwahudumia walengwa tajwa.

Hiyo inajionyesha namna, akiwajibisha timu ya sekretarieti ya chama kuwajibika jamii, kutoa msukumo wa watendaji wa umma kutumikia jamii.

Vilevile ni kwa namna pekee, kunaibuliwa haja ya kufikia haki za wakulima ambao ndio idadi kubwa ya Watanzania katika kuchangia uchumi, hali kadhalika eneo hilo likitoa ajira ya umma.

**DEMOKRASIA NA MARIDHIANO**

Katika sura ya pili, kwenye eneo la haki lililoainishwa kwenye Ilani ya Uchaguzi ya CCM, 2020 hadi 2025, kunashuhudiwa uamuzi wa kiserikali kutoka kwa Rais Dk. Samia, ambaye pia ni mwenyekiti akifanya uamuzi mzito kitaifa, anagusa mambo kadhaa ya kidemokrasia.

Hapo kunatajwa Dk. Samia kufikia uamuzi mzito kuhusu kufuta mashitaka kwa baadhi ya wanasiasa wa upinzani, wakiwamo waliokuwa rumande.

Ni hatua iliyoendana na michakato, pia mijadala ya maridhiano, mojawapo akishuhudiwa Mwenyekiti wa CHADEMA, Freeman Mbowe, siku moja baada ya kufutiwa mashitaka na kuachiwa huru kutoka rumande gerezani, akapata faragha na Rais Samia, kujadili nyendo za demokrasia kitaifa.

Faragha kama hiyo, pia ilimfika makamu wake Mbowe, Tundu Lissu jijini Brussels, alikokimbilia baada ya kunusurika kifo nchini akishambuliwa kwa risasi na wasiojulikana.

Huko jijini Brussels Ubelgiji, Lissu wakateta na Dk. Samia aliyekuwa ziarani kikazi hata. Leo matunda yanashuhudiwa, Lissu amerejea nchini kwa zaidi ya wiki moja na sasa anashiriki mikutano ya kisiasa.

Vivyo hivyo, Godbless Lema, aliyekuwa mbunge wa Arusha Mjini (Chadema) aliyekimbilia nchini Canada, akiondoka na familia yake tangu mwaka 2020, naye anaungana nao akitangaza kurejea nchini wiki nne zijazo katika staili ya uamuzi kama wa Lissu.

Ni haiba ya siasa za maridhiano kutoka mzizi wa siasa na ustawi wa jamii, ambao mwenyekiti huyo wa CCM ameyafungulia kupitia ufunguo wa kirais, huku akipewa hongera na baraka za CCM.



Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, katika mizunguko ya kisiasa ya CCM.

Hatua ya mwisho iliyofikiwa sasa mezani, ni vilio vikuu vya vyama vya upinzani; katiba mpya iliyoahidiwa kufanyiwa kazi na Rais Samia, pia mikutano ya hadhara ambayo tayari nuru imeendelea kumea nchini, wananchi wakishiriki.

Ukamilifu wa ushuhuda ukajikita pale viongozi mbalimbali wa kambi ya upinzani kwa uwazi wakipongeza uamuzi huo, kila mmoja kwa nafasi yake; mikutano na waandishi wa habari, mikutano ya kisiasa na mitandao ya kijamii.

Katika mkutano wake huo wa kufungua ulingo wa kidemokrasia na maridhiano Ikulu jijini Dar es Salaam, Rais Samia aliruhusu kukosolewa kisiasa, lakini kwa angalizo lake ni kwamba, kuwapo mazingira ya kistaha na yanayotoa msukumo kwa serikali yake kuwajibika zaidi.

**AFUNGAMANA NA ILANI**


Ndani ya serikali ya CCM iliyopo sasa, siasa inayotawala iko wazi ni zao la kazi ya Rais Dk. Samia, ambaye kwa nafasi yake ya uenyekiti wa CCM, anaelekezwa na Ilani ya Uchaguzi anayoitumikia sasa, kati ya mwaka 2020 hadi 2025 ikimtamkia katika Sura ya 118:

"Katika kipindi cha miaka mitano ijayo, Chama Cha Mapinduzi kitaendelea kuheshimu na kulinda misingi ya demokrasia na haki za binadamu kwa ajili ya ustawi wa Taifa kwa kuzingatia Katiba ya Tanzania.

"Lengo la Chama Cha Mapinduzi katika kipindi hiki, ni kuhakikisha kuwa wananchi wanaendelea kupata haki kwa mtu mmoja mmoja na makundi mbalimbali," inaeleza ilani hiyo.

Katika kipengele 'c' cha sura hiyo, inafafanuliwa zaidi kwamba: "Kubuni na kutekeleza mikakati ya kukuza, kulinda na kutekeleza misingi ya haki za binadamu na wajibu wao (umma)."

Pia, kipengele 'e' kina matamshi "kuweka mazingira wezeshi ya haki kwa wananchi kushiriki katika shughuli mbalimbali za kiuchumi, kijamii na kisiasa."



Mzee Ali Hassan Mwinyi; Mwenyekiti wa pili wa CCM.

**ULINGO WA HAKI**

Katika staili yake ya serikali kutimiza matakwa ya utashi wa CCM mbali na misamaha ya kisheria kwa mtu mmoja mmoja, amekuwa akikosoa suala la utendaji haki ndani ya vyombo vya dola katika mifumo ya kisheria tangu kuingia madarakani.

Zito lililochukua sura wiki hii, ni pale alipokosoa tena baadhi ya maeneo ya kiserikali, akinyooshea kidole utendaji wa baadhi ya vyombo vya dola na kisheria katika kusimamia haki ya umma.

Hapo akachukua hatua wiki hii ya kuzindua chombo alichounda karibuni, cha kufanya mapitio kuhusu ufanisi wake kimuundo kwenye vyombo vya dola, akijumuisha baadhi kama Polisi, Magereza, Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashitaka (DPP), Taasisi ya Kudhibiti na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU).

Ni uamuzi mwingine unaoegemea katika Sura ya 110 Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020 - 2025, inayoelekeza kuimarishwa taasisi za utawala bora, maadili na uwajibikaji, ikitoa mfano mmojawapo Tume ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya .

**UENDESHAJI CHAMA**

Kwa kiongozi kuendesha taasisi yoyote ikiwamo chama cha kisiasa, huwa anasimamiwa na mambo kadhaa, lakini muhimu zaidi ni miongozo mikuu ya kitaasisi, pia umma.

Hapo kunatajwa sera na sheria kitaifa na kimataifa, ikishuka pia katika ngazi ya kitaifa. Vilevile, kuna miongozo ya ndani kitaasisi; sheria, sera na maelekezo. Hapo nako kuna la ziada linaloegemea utashi binafsi wa kibinadamu.

Mara zote utashi huangukia tofauti kati ya mtu mmoja na mwingine, ingawa bado wote wanafungwa na miongozo mikuu tajwa, matendo ya kiuongozi yasitoke nje ya ulingo.

Kama alivyo mwanazuoni wa sayansi ya siasa, Harold Laswell alipofanya utafiti, akaangukia na majibu kwamba: "Siasa ni mchakato wa nani anapata nini, lini na kwa namna gani". Katika mtazamo mkuu kinacholengwa hapo huwa ni mamlaka ya kusimamia na kugawanya rasilimali iliyoko katika jamii husika.

**INAENDELEA UK. 5**

MAKALA



Viongozi wa CCM katika moja ya mikutano yao ya kitaifa.

# Sura ya CCM mpya chini ya Rais Samia

INATOKA UK. 4

Ikirejewa mustakabali wa uongozi ndani ya CCM, ambayo nayo kama chama tawala chochote duniani, inasimamia nyendo za kitaifa, pia utashi wa kiongozi aliyepo.

Hivyo, katika mfumo na utashi wa Rais Samia, unaegemea zaidi namna shirikishi, pia maridhiano kijamii. Uhalisia wake ukijionyesha siku za kwanza za uongozi wake, akapitisha ajenda ya chama, pia katika kofia yake ya urais, akiweka ajenda na vikao vya maridhiano na wanasiasa mbalimbali.

Ni hali iliyojenga busara na utashi wa kirafiki kutoka kila pande za kisiasa, hata kupooza hali ya msuguano wa kisiasa kitaifa, ikiwamo kati ya CCM na vyama vingine.

Mantiki ya uendeshaji siasa ya Rais Samia ilionekana hata kutoka upande wa pili wa Jamhuri mapema kabla ya kuteuliwa kuwa rais, akiwa makamu wa rais.

Rais wa Zanzibar, ambaye pia sasa ni Makamu Mwenyekiti wa CCM (Zanzibar), akaanza kwa kuisisitiza 'kutokalia siasa za kufukua makaburi (ya msuguano).'

Nako kumeshuhudiwa amani na maridhiano kati ya CCM na chama pinzani CUF, ambayo wadau wake wengi sasa wako kwenye joho la ACT - Wazalendo, kukishuhudiwa ukaribu kisiasa wa kihistoria kwa viongozi wa serikali ya pamoja visiwani; Rais Dk. Mwinyi na Makamu wa Pili, marehemu Maalim Seif Shariff Hamad, ikiendelea hata kwa mrithi wa sasa.

Kwa kiasi kikubwa nyendo za kisiasa za Rais Samia hadi sasa, ni za sura hiyo, hata kunaonekana kuwa ndivyo ilivyo serikali ya CCM kitaifa. Marejeo hayo yamejitokeza hata alipokutana na uongozi wa vyama 19 vya siasa nchini, kuwapa majibu ya kiserikali juu ya kilichoamuliwa.

Hapo akafafanua: "Ili taifa liwe moja, lazima tuwe na maridhiano, nikasema kwanza tuwe na mazungumzo kwenye vyama vya siasa..."

Pia ananena: "Wakati mnanikabidhi kuongoza nchi hii, busara zilinituma kwamba jinsi nilivyolipokea taifa hili, kuna haja ya kufanya taifa liwe kitu kimoja, wote tuzungumze lugha moja."

Rais Samia ameeleza kwamba kikosi kazi alichounda na kumletea maoni kwenye maeneo tisa, anadokeza makubwa matatu yaliyoanikwa ni; kutaka kuruhusiwa mikutano ya hadhara ya vyama vya siasa, mchakato wa katiba mpya na marekebisho ya sheria mbalimbali.

Anasema, tayari michakato ya marekebisho ya sheria imeshaaanza na waziri mwenye dhamana anaifanyia kazi na itatolewa taarifa itakapotimu, huku dai la marekebisho ya katiba nchini, akikubaliana nalo, akiahidi litafanyiwa kazi kulingana na mazingira yatakayojiri.

Ni kikao kilichohudhuriwa na Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, pia wenyeviti, makatibu wakuu na manaibu katibu wakuu wa vyama vyote 19 vya siasa vyenye usajili wa kudumu nchini; UPDP, NRA, TADEA, TLP, CHADEMA, CUF, NCCR Mageuzi, UDP na UMD, CCM, Demokrasia Makini, DP, SAU, AFP, CCK, ADC, CHAUMMA na ACT- Wazalendo.



Jakaya Kikwete; Mwenyekiti wa nne CCM.



Hayati Benjamin Mkapa; akiwa wa tatu, nafasi ya uenyekiti wa CCM.

**MKULIMA & MWANAMAMA**

Alama kuu ya CCM ni Jembe na Nyundo, zikiwakilisha mkulima na mfanyakazi. Ni dhana ya urithi tangu vyama watangulizi- TANU na ASP, ikifahamika kwamba kilimo ndio mwajiri na mzalishaji mkuu katika uchumi wa taifa.

Ilani ya Uchaguzi ya CCM imatumika sasa, Sura ya 37 inathamini hilo kwa kuielekeza serikali kuwekeza kwa kiasi kikubwa katika kilimo cha kisasa, ikiwamo mapinduzi ya umwagiliaji na udongo bora.

Ni hatua inayojithibitisha kurejea kiashiria cha 'jembe' pale serikali inayoongozwa na Rais Samia, kuja na makadirio ya mapato na matumizi (bajeti) yenye mapinduzi makubwa katika kilimo, kutoka Sh. 294, 162, 071, 000 katika bajeti iliyopita hadi Sh. 751,123, 280,009 za sasa.

"Katika kipindi cha miaka mitano ijayo, Chama Cha Mapinduzi kitaendelea kusimamia mapinduzi ya kilimo ili kuhakikisha kinaendelea kuwa chenye tija na kinachotumia teknolojia ya kisasa.

"Aidha, chama kitahakikisha kuwa Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili (ASDP II) inaendelea kutekelezwa na kutoa mchango mkubwa katika usalama wa chakula, pato la Taifa, maendeleo ya sekta ya viwanda na huduma kwa kutekeleza," inatamka sehemu ya Ilani yake.

Pia, angalizo jingine, ni hadi sasa ndani ya uongozi wa chama – CCM, serikali na taasisi mbalimbali za umma, nafasi ya uwakilishi wa mwanamke umekuwa dhahiri chini ya uongozi wa Rais, ambaye ana kofia mbili za ukuu kichama na serikali, kimataifa aking'ara 'ni mama wa mfano.'



Hayati John Magufuli; Mwenyekiti aliyemuachia kijiti Rais Samia Suluhu Hassan. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# CCM inastahili pongezi kwa kutimiza miaka 46

**FEBRUARI** 5, 1977 lilitokea tukio kubwa katika siasa za Tanzania. Tukio hilo ni la kuzaliwa kwa Chama Cha Mapinduzi (CCM) kutokana na kuunganishwa kwa vyama vya TANU na Afro Shiraz Party (ASP) ambavyo vilishiriki harakati za kuondoa ukoloni nchini na hatimaye kufanikisha kupatikana kwa Uhuru wa Tanganyika mwaka 1961 na Mapinduzi matukufu ya Zanzibar mwaka 1964.

Pamoja na kwamba vyama hivyo viliendelea kutawala pande zote za Muungano tangu mwaka 1964, viongozi wao waliona ni busara kuviunganisha na kuanzishwa chama kipya ambacho kilichukua mila, desturi, miiko na ahadi za vyama vya awali. Kuunganishwa kwa vyama hivyo kulikusudia pia kuwa na chama chenye nguvu kitakachotoa mwongozo na msukumo wa kimaendeleo kwa serikali zote za Muungano na Zanzibar.

Hadi sasa, ni miaka 46 tangu chama hicho kilipoanzishwa kutokana na busara za aliyekuwa mwenyekiti wa TANU na Rais wa Tanzania, Mwalimu Julius Nyerere na mwenzake Alhaj Aboud Jumbe Mwinyi, aliyekuwa Mwenyekiti wa ASP, Makamu wa Rais wa Tanzania na Rais wa Zanzibar.

Kimsingi, sababu za kuungana kwa vyama hivyo, hazikuwa tofauti na zile zilizofanya Tanganyika na Zanzibar kuungana na kuwa na taifa moja imara, lililopewa jina la Tanzania. Miongoni mwa sababu hizo ni udugu wa asili baina ya watu wa mataifa hayo uliokuwapo hata kabla ya ukoloni pamoja na mila na desturi zao. Lakini kubwa zaidi, ni kuwa na chama kimoja chenye nguvu kwa ajili ya kuzisimamia serikali katika kuwaletea wananchi maendeleo.

Ikiwa imetimia miaka 46 tangu kuanzishwa kwa CCM, yako mambo mengi yaliyofanywa yakiwamo kutoa dira na miongozo kwa ajili ya maendeleo ya kisiasa, kiuchumi na kijamii na utekelezaji wa miradi ya maendeleo kupitia ilani za uchaguzi zinazoandaliwa kila wakati wa uchaguzi.

Katika miaka yote hiyo, CCM imeonekana kuwa chama bora chenye kupigiwa mfano na vyama vyote vya siasa ndani na nje ya nchi. Jambo la kwanza, ni kujipambanua kuwa ni chama cha kidemokrasia kwa vitendo kutokana na kufanya mabadiliko ya uongozi kwa kufuata katiba yake na kanuni ilizojiwekea.

Tangu kuasisiwa kwake, viongozi wamekuwa wakiingia na kutoka kwa mujibu wa katiba na hata aliyejaribu kupindisha utaratibu huo, alishughulikiwa ipasavyo. Rais wa Muungano au wa Zanzibar anayetokana na CCM, anakaa madarakani vipindi viwili vya miaka mitano kila kimoja na baada ya hapo anateuliwa mwingine kugombea nafasi hiyo.


Licha ya kuwapo kwa utaratibu huo ngazi za kitaifa, CCM pia ina utaratibu wa kufanya uchaguzi kuanzia ngazi ya shina kila baada ya miaka mitano na upatikanaji wa wagombea katika nafasi mbalimbali hufanyika kwa kufuata kanuni na taratibu na hatimaye demokrasia kuchukua mkondo wake.

Kadhalika, katika kuhakikisha inaendeleza imani yake kwa wananchi, CCM imekuwa ikitekeleza ilani zake za uchaguzi katika sekta mbalimbali kama vile ujenzi wa miundombinu, afya, kilimo, mifugo, maji na elimu. Kubwa zaidi, imekuwa ikisisitiza umoja, amani na mshikamano ambavyo ni muhimu katika upatikanaji wa maendeleo endelevu.

Kama alivyosema Nyerere kwamba bila CCM madhubuti nchi itayumba, ni dhahiri kwamba chama hicho kimesimamia misingi ambayo imesababisha nchi kuwa imara katika nyanja mbalimbali na hata kuwafanya Watanzania kuendelea kukiamini na kukichagua kila uchaguzi mkuu unapowadia. Kwa kutimiza umri huo, CCM inastahili kupongezwa na shime iendelee kuzisimamia serikali zake kuwaletea wananchi maendeleo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Adhabu ya viboko katika shule itutafakarishe zaidi

Na Sabato Kasika

**KUWAPO** au kutokuwapo kwa adhabu ya viboko shuleni, ni mjadala wa muda mrefu ambao umekuwa ukijadiliwa mara kwa mara na wadau wa elimu, wakiwamo wanaoipinga adhabu hiyo na wengine kuikubali.

Wanaopinga adhabu hiyo wanadai kuwa wakidai kuwa imegeuka kuwa mateso kwa wanafunzi badala ya kusaidia kuwarekebisha, lakini wanaotaka iendelee kuwapo, wanadai kuwa inasaidia kunyoosha wanafunzi wakorofi.

Binafsi ninaona kwamba, sababu zote zina mashiko, kwani ni kweli kwamba baadhi ya walimu wamekuwa wakitoa adhabu ambazo ni kama mateso, lakini pia ni kweli wako baadhi ya wanafunzi wasipochapwa wanaweza kuharibika.

Jambo la kutazamwa hapa ni kuwaweka sawa walimu ili wasiendelee kuonekana kama watu wakatili, hasa kutokana na ukweli kwamba, baadhi yao wamekuwa kama wanakomoa wanafunzi.

Baadhi yao wamekuwa wakisababisha madhara makubwa kwa wanafunzi kutokana ba adhabu za viboko wanazotoa. Hivyo ninadhani yapo mambo kadhaa ya kufanya ili kutuliza hali ya hewa.

Mojawapo ni kuangalia haki za walimu na wajibu wao katika malezi ya wanafunzi, huku wizara yenye dhamana ya elimu ikisimamia mwongozo wa adhabu shuleni kupitia waraka wa elimu namba 24 wa mwaka 2002.

Ikumbukwe kuwa miongoni mwa maelekezo ya waraka huo, ni kwamba viboko vitatolewa kwa ajili ya makosa makubwa. Makosa hayo yanatajwa kuwa ni uvutaji wa bhangi, wizi wanafunzi kupigana na pia uharibifu wa mali za shule na za wenzao.

Lakini pia waraka huo unaelekeza kuwa mwalimu mkuu ndiye mwenye mamlaka ya kuruhusu kimaandishi au mwenye kutoa adhabu hiyo, na kwamba viboko visizidi vinne na viandikwe katika kitabu cha kumbukumbu na si vinginevyo kama inavyofanyika.

Labda nikumbushe tu kuwa dunia imekuwa kama kijiji baada ya kupanuka kwa teknolojia, hivyo imekuwa ni rahisi kupata taarifa za matukio mbalimbali yakiwamo hayo ya baadhi ya kutoa adhabu kinyume na mwongozo.

Matukio ya kikatili dhidi ya wanafunzi, yanayoitwa adhabu, ndio ambayo yanasababisha kuwapo kwa mjadala wa muda mrefu wa au adhabu hiyo ya viboko iendelee kutolewa ama ifutwe.

Ninaamini kuwa kama mwongozo ungefuatwa, adhabu ambazo ni kama kukomoa wanafunzi zisingekuwapo, lakini kwa sababu bado wapo baadhi ya walimu wanaofurahia mateso hayo, wasaidiwe ili waachane na mtindo huo.

Njia mojawapo ya kuwasaidia, ni kuhakikisha miiko na maadili ya walimu vinahuishwa, ili walimu wanaoshidwa kuzuia vitendo vya ukatili kwa wanafunzi wachukuliwe hatua za kisheria.

Ninashauri hayo kwani jamii imekuwa ikishuhudia wanafunzi wakichapwa viboko kinyume na taratibu, huku baadhi ya walimu wengine wakifurahia, wakiamini kuwa wanachokifanya ni sahihi.

Vilevile, ni vyema walimu waandamizi wakatumika kuwasaidia walimu wengine kuimarisha stadi zao za maisha na uwezo wa kukabiliana na vitendo viovu vya baadhi ya wanafunzi.

Lakini pia si vibaya walimu wakapata mafunzo mbalimbali na kozi maalumu ya jinsi ya kuwafundisha wanafunzi wenye matatizo ya kitabia na utoaji wa adhabu chanya, ili kuepuka kuingia katika matatizo.

Suala la mafunzo kazini kwa walimu, nalo lingepewa uzito, hasa mafunzo yanayohusisha utoaji wa adhabu chanya na jinsi ya kuwarekebisha wanafunzi wenye matatizo ya kitabia.

Pamoja na hayo, wazazi, walezi na walimu, ni vyema washirikiane katika malezi, kwani kila upande una nafasi yake katika malezi, ingawa baadhi ya wazazi na walezi, hutuhumiwa kutoshirikiana na walimu.

Kutokuwapo kwa ushirikiano na walimu, kunaweza kuchangia watoto wao kuharibika na kufanya matendo maovu shuleni bila wazazi wenyewe kujua na kujikuta wakilaumu walimu na kumbe chanzo cha tatizo ni wao.

FIKRA MBADALA

# Inahitajika elimu kwa umma kuhusu katiba, sheria, haki



Pascal Mayalla

MAKALA ya leo inahusu haki za binadamu. Kwa wale wenye kumbukumbu nzuri ya safu hii, makala za mwanzo kabisa zilikuwa "kilio cha haki" ambazo nilizungumzia sana haki jinai. Kwa mantiki hiyo, kauli thabiti za Rais Samia Suluhu Hassan katika utoaji haki, nimeanza kuzifuatilia kwa muda mrefu na wiki hii amezitoa tena katika matukio makubwa mawili. Tukio la kwanza ni wakati wa uzinduzi wa Tume ya Haki Jinai jijini Dodoma Jumatatu iliyopita na tukio la pili ni Siku ya Sheria.

Kwenye utetezi wa haki nchini Tanzania, tukubali tukatae, Rais Samia ana nia njema na ya dhati ya kuhakikisha Watanzania wanatendewa haki kwenye vyombo vya utoaji haki. Moja ya udhaifu mkubwa katika utoaji haki Tanzania ni Watanzania kutozijua haki zao.

Haki hailetwi kwenye kisahani cha chai bali ni stahili na stahiki inayopaswa kutolewa bila kuiomba na ikitokea haki haikutolewa au haikutendeka. Haiombwi, hivyo hupaswi bali inapaswa kudaiwa. Sasa ukiwa hujui haki yako, huwezi kudai kitu usichokijua.

Hiki kitu cha Watanzania kutokujua haki zao, nimesikitena wiki hii Rais Samia akirudia kukisema kwenye kilele cha siku ya sheria iliyoadhimishwa kitaifa uwanja wa Chinangali, jijini Dodoma. Rais Samia alisema mambo mengi makubwa mazuri katika utoaji haki nchini Tanzania, kubwa nililoondoka nalo ni hili la Watanzania kutojua haki zao.

Kwenye hili, Rais Samia amesema na ninamnukuu: "Wanasema, kuna msemo maarufu kwamba haki hupewi mkononi, lazima uitafute. Lakini katika kutafuta haki kuna ujuzi, wananchi wetu wengi hawana ujuzi wa kutafuta haki zao kwa hiyo tuwasaidie kutafuta au kupata haki zao."

Hii si mara ya kwanza kwa Rais Samia kuzungumzia changamoto ya haki kwa Watanzania wengi wasiojua haki zao. Mwaka jana siku ya maadhimisho ya miaka 10 ya Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binaadamu Tanzania (THRDC) inayoongozwa na mwanasheria Onesmo Olengurumwa, Rais Samia alisema: "Mtetezi mkubwa wa haki za binadamu ndani ya Tanzania ni Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambayo serikali ndiyo inaitekeleza. Ndiyo sheria mama ambayo inaainisha haki zote za binadamu wanaoishi Tanzania.

Rais Samia anaendelea: "Suala langu kwenu ni je, hawa wanadamu tunaowatetea, wanaijua hiyo Katiba? Na nataka niache kazi kwenu katika eneo la elimu kwa umma, muifanye kazi hii ya kuwaelekeza watu waijue katiba yao kwa sababu wanapodai haki, lazima wajue na wajibu wao. Haki ziko kwenye katiba na wajibu uko kwenye Katiba. Wakielekezwa vizuri wataujua na wajibu wao nini kikatiba."

Kwa hiyo, makala hii inachokifanya ni kuwaelimisha Watanzania kuhusu haki zao na Katiba yao. Ni kuwasaidia Watanzania, kulisaidia taifa na kumsaidia Rais Samia. Natoa wito kwa wanasheria kote nchini, haijalishi wewe ni nani kuanzia Jaji Mkuu, majaji, mahakimu, mawakili na wasaidizi wa sheria na bila kujali uko mahakamani, serikalini, taasisi za umma, mashirika au wanasheria binafsi, tukiwamo sisi mawakili, kumuunga mkono Rais katika kutimiza azma njema ya kuhakikisha Watanzania wanatendewa haki.

Tume hiyo ya haki jinai inayoongozwa na Jaji Mkuu mstaafu Othman Chande, akisaidiawa na Katibu Mkuu Kiongozi mstaafu, Balozi Ombeni Sefue, imepewa miezi mine kuangalia mifumo ya utendaji wa taasisi zote za utoaji haki na kuahidi kuyafanyia kazi matokea ya tume hiyo, yakiwemo lile "zumari" fulani ambalo Jaji Mkuu Prof. Ibrahim Juma, alilizungumzia kuwa lilipigwa kutokea Zanzibar, mlio wake ufike na huku Bara.

Rais Samia amesisitiza kwa vile na yeye ametokea Zanzibar akasema: "Lile zumari litalia na mimi ni Mpemba, najua sana kupuliza zumari, kwa lile zumari litapulizwa. Nitakapopokea taarifa ya tume na kusema ndiyo mama puliza zumari, nitakwenda kufanya hivyo." Kwa hiyo sasa taasisi za haki pingeni kongole sana kwa Rais Samia kusikia kilio chenu kilichowasilishwa kwake na Jaji Mkuu Prof. Juma. Sasa kaeni mkao wa kula.

Kauli za vingozi wa kisiasa zinazotolewa kwenye hotuba, ziko za aina mbili. Kwanza kiongozi anaandikiwa hotuba, kisha anapewa kuipitia. Katika kuipitia huko, huongeza yale yake ya moyoni ambayo hakuandikiwa, Pili, inawezekana hayo aliyoandikiwa, akakubaliana nayo na kuyaingiza maoni yake, hivyo akihutubia yanakuwa yake.

Sisi wasikilizaji wa hotuba za viongozi pia tuko wa aina mbalimbali. Kuna baadhi yetu tumejaliwa uwezo wa ziada na unaposikiliza hotuba ya kiongozi, unakuwa na jicho la rohoni na sikio la ndani. Kiongozi akisoma hotuba aliyoandikiwa, lakini anayoyasoma hayatoki moyoni kwake, baadhi yetu tunajua.

Kiongozi anayesoma hotuba aliyoandikiwa, huku hayo anayoyasema hayatoki moyoni, bali yanatoka mdomoni tu, wenzetu wazungu wanaita kwa Kiingereza, "paying lip services". Kuna wanasiasa wengi wanatoa hotuba za kuandikiwa au hata bila kuandikiwa, bali wanasema kile kitu watu wanachotaka kusikia lakini hakitoki mioyoni mwao. Ndio maana kwenye mikutano mingi ya kampeni, wanasiasa wanaahidi vitu vingi, vingine ni vya uongo au vya kweli lakini havitekelezwi!

Nikimwangalia Rais Samia,na kusikiliza kauli zake katika hili la haki, kusema ukweli kabisa, ana nia ya dhati kutoka moyoni mwake kuhakikisha Watanzania wanatendewa haki. Kauli za Rais Samia kuhusu haki si 'playing lip services' bali anamaanisha kabisa hicho anachozungumza.

Kuna maneo katika maandiko matakatifu kwamba "haki huinuia taifa, bali dhambi ni aibu kwa wowote". Kwa hiki anachokifanya Rais Samia kwenye utoaji wa haki Tanzania, ataliinua sana taifa la Tanzania, hivyo atabarikiwa na Tanzania itabarikiwa sana.

**Mungu Mbariki Rais wetu Samia**

MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO

# Hili la idadi ya wachezaji wa kigeni lisipoangaliwa...



Na Joseph Kulangwa (kulangwasos@gmail.com)

MIAKA ya nyuma Tanzania ilijivunia kuwa na wachezaji wazuri wa soka katika ngazi ya klabu na Taifa, wakililetea Taifa heshima na sifa nyingi katika medani ya mchezo huo.

Majina kama Abdallah Kibaden, Maulid Dilunga na Sunday Manara, yalikuwa maarufu kitaifa na kimataifa, hata baadhi yao kuchaguliwa kuchezea timu ya Afrika (Kibaden, Dilunga) huku Sunday akicheza Ughaibuni.

Timu ya Taifa, Taifa Stars, ilishiriki michuano ya kimataifa barani Afrika na kufika ngazi za juu huku ikizishinda nchi kubwa kubwa kisoka, kama vile Nigeria, Zambia na zingine hata kufika fainali.

Tanzania ilikuwa na uwezo huo kwa kutumia wachezaji wake wa ndani, bila kuwa na wa kutoka nje ya nchi kama ilivyo sasa na ilipotokea, ilikuwa nadra na idadi ya wachezaji wakiwa wachache sana.

Mmoja wa wachezaji hao maarufu ni Nonda Shabani, raia wa Zaire (sasa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo-DRC), aliyecheza Yanga na baadaye akaenda Afrika Kusini na hatimaye kumalizia soka lake Ulaya.

Wakati Nonda akicheza nchini, mchezaji wa zamani wa Yanga, Sunday alikuwa ughaibuni akiwa mchezaji wa kwanza Mtanzania kucheza nje ya nchi kwa mafanikio makubwa na kufuatiwa na mdogo wake, Kassim Manara.

Uwezo wa wachezaji enzi hizo nchini ulikuwa mkubwa katika timu za Yanga, Simba, Nyota Nyekundu, Pan Africa, Mseto, Tukuyu Stars, Pamba, Cosmopolitans, Toto Africa na zingine, huku zikitoa wachezaji waliounda Taifa Stars na kucheza kwa mafanikio makubwa.

Hilo liliwezekana, kwa kuwatumia katika mechi mbalimbali za ngazi za klabu na hata Taifa na hivyo kujijengea ujasiri na imani hata kukabiliana na klabu zingine za kimataifa, zilizokuja nchini na hata zilizofuatwa zilikokuwa.

Haikuwa ajabu kwa timu ya Tanzania kwenda nje na kurudi na ushindi, lakini hata kukabikiana na nchi hizo za kigeni na kuzishinda kirahisi na kuiletea nchi sifa kubwa kimataifa.

Siku zilivyozidi kusonga mbele, nchi ikaanza kuruhusu wachezaji wa kigeni kuja kusajili kwa idadi fulani, ambapo mpaka sasa klabu zinazoshiriki ligi mbalimbali nchini, zinaruhusiwa kusajili hadi wachezaji 12 wa kigeni. Timu nzima na mmoja wa ziada.

Kutokana na ongezeko la wacheaji hao wa kigeni, ambalo baadhi wanadai kuwa ni kuwapa changamoto wazawa ili wajitume zaidi, kinachoonekana ni kuwa hivi sasa wamefifia na kuacha wageni kung'ara.

Kufifia huko pia kumeifanya timu ya Taifa kunyongea na kushindwa kufanya vizuri katika michuano ya kimataifa husussan Afrika-kwenye CHAN na mingine, kutokana na kushindwa kuchuana na wageni.

Hivi sasa timu zote zinazoshiriki Ligi Kuu ya soka nchini, zina wachezaji wa kigeni kutoka DRC, Zambia, Malawi, Senegal, Mali, Ivory Coast, Ghana, Nigeria, Kenya, Uganda, Rwanda na Burundi.

Wachezaji galacha ni wale wa kigeni katika timu hizo, huku wazawa wakionekana wasindikizaji wasioonekana kufanya vizuri katika timu zao, kutokana na wageni waliopo na vivyo hivyo kushindwa kuchangia vizuri katika timu ya Taifa.

Timu za Tanzania zinatumia fedha nyingi sasa kusajili wachezaji wa kigeni na kuwalipa mishahara mikubwa tofauti na wazawa wenye kiwango cha juu cha uchezaji na hata kuwavunja moyo.

Hili lilijidhihirisha hivi karibuni kwa mchazaji wa Yanga, Feisal Salum 'Fei Toto', anayelipwa kiwango kidogo cha mshahara kulinganisha na wachezaji wa kigeni wasiomfikia kiwango.

Wachezaji hao, baadhi yao walishastaafu kuchezea klabu na timu za Taifa za nchi zao na hivyo kutafuta mahali pa kustaafia na kuziba fursa za wachezaji wetu kukua kisoka, na kutoa mchango kwa klabu na Taifa lao.

Kama tusipoangalia, tukaendelea kukumbatia wachezaji wa kigeni tena kwa idadi hiyo au zaidi, hatutakaa kushinda katika soka la ngazi ya kimataifa, kwa kuwa wachezaji wetu wanadumazwa na mfumo uliopo. Hiyo ndiyo hali inayoikuta England leo, inayokumbatia wageni kuliko wazawa. Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo isipokuja na ubunifu, tutaendelea kukwama. **Alamsiki!**

# Wakulima wagomea malipo ya kahawa

**Na Mary Mosha,** MOSHI

WAKULIMA wa Chama cha Msingi cha Ushirika cha Mwika Msae Kinyamvuo cha wilayani Moshi mkoani Kilimanjaro wamekataa kupokea malipo ya 797 kwa kilo ya kahawa kutoka Chama Kikuu cha Ushirika mkoani Kilimanjaro (KNCU) wakidai kulipwa kiasi Sh. 11,250 kwa kilo kama walivyokubaliana katika mkataba na mwekezaji.

Glory Sam, mmoja wa wakulima hao, alidai jana kuwa katika kikao maalumu cha kujadili madai ya wakulima, mwanzoni walikubaliana kahawa yao itauzwa kwa mwekezaji huyo na alikubali kuinunua kwa Sh. 11,250 kwa kilo.

"Wamekuja hapa mara kadhaa wakituambia tutapokea Sh. 300 kwa kilo moja na baada ya malalamiko ya muda mrefu na ushirikishwaji wa viongozi wa serikali kwa ngazi ya wilaya, wakaja leo na bei ya Sh. 797, huku wakisema mwekezaji alitoroka wakati hili jambo sio kweli," alidai.

"Kahawa yetu ni 'organic', wao wanadai waliiuza kwenye mnada baada ya mwekezaji kukimbia, jambo ambalo hawakutushirikisha. Hii sisi hatukubali na hatuna imani na chama hiki tena, hivyo tunamwomba Waziri Mkuu kwa kushirikiana na Waziri wa Kilimo kutusaidia kufanya uchunguzi wa kina, kwani hawa wamekuwa sehemu ya kudidimiza ushirika," alisema Fatael Mgasi.

"Maelezo wanayotoa KNCU ni kosa kisheria, wameingia mkataba na kukubaliana kuwa watalipa Sh. 11,250, kwa kilo. Leo wanakuja na hesabu za Sh. 797, hatutachukua hiyo fedha, bora wabaki nayo watuletee kahawa yetu, tutang'oa miche yote tuoteshe parachini na mazao mengine yanayoweza kuleta matokeo chanya baada ya kuyagharimia," alidai Mch. Mbuya.

Mary Sebastian, mkulima na Mwenyekiti wa Kitongoji cha Chona anadai kuchelewa kwa fedha hizo kumechangia wananchi kutoshiriki kwenye michango ya maendeleo ikiwamo ya elimu. "Asilimia 70 ya wananchi wa kitongoji changu ni wakulima wa kahawa, wameshindwa kupeleka watoto wao shuleni kwa kushindwa kukindi mahitaji yao, wakisubiri fedha zao za mauzo ya kahawa.

"Na wengine wamekopa maeneo mbalimbali zikiwamo taasisi za fedha ili wajikimu," alidai mwenyekiti huyo.

Kaimu Mwenyekiti wa chama hicho, Israel Kombe alidai kuwa baada ya usumbufu wa muda mrefu, walipata mkataba uliotiwa saini na viongozi wa KNCU na mwekezaji kutoka Kampuni ya Continental Trade and Commodity Servive- CTCS Julai 27, 2022 ambaye alikuwa tayari kuwalipa wakulima Sh. 11,250.

Godfrey Massawe, Kaimu Meneja wa KNCU, alisema kwa sasa wakulima wanapaswa kulipwa Sh. 797 licha ya kuwa tayari mwekezaji kutoka kampuni ya Continental Trade and Commodity Servive alishatoa gharama ya awali ya Sh. milioni 300.

Akitoka kauli ya seriklali, Mwakilishi wa Mkuu wa Wilaya ya Moshi, Senzia Lushino alimwagiza mraji msaidizi wa wilaya kuunda timu ya kufuatilia malalamiko ya wakulima zikiwamo hesabu zinazolalamikiwa baada ya kuondoka kwa mwekezaji huyo.

"Wakague kwanini kahawa imeuzwa kwa bei ya chini, uhalali wa hesabu pamoja na kwanini mwekezaji alikimbia ili kuona ikiwa kuna usumbufu wowote waliousababisha wao au kuna sababu nyingine, na ripoti yao itatusaidia kushirikiana kwa pamoja ni nani aliyeleta hasara na aweze kuwajibika," aliagiza.



Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wazazi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) kata ya Wazo, Jesca Mrope, akipanda mti wa matunda huku akisaidiwa na Mwenyekiti wa CCM wa kata hiyo, Abdallah Mbondela (kushoto), wakati wa tukio la upandaji miti lililoandaliwa na jumuiya hiyo, katika Shule ya Sekondari Songoro Mnyonge, Kilimahewa Juu, Manispaa ya Kinondoni, Dar es Salaam jana, wakiadhimisha miaka 46 ya kuzaliwa kwa chama hicho. Miti 200 ya matunda na kivuli ilipandwa katika shule hiyo, kituo kipya cha afya kinachojengwa Nyakasangwe na Mahakama ya Mwanzo ya Nakarekwa. Wanaoshuhudia ni Katibu wa Wazazi wa kata hiyo, Rehema Salama (nyuma yao) na viongozi mbalimbali wa jumuiya na chama. **PICHA: JOHN BADI**

# Tundu Lissu afichua siri alivyopigwa risasi

**Na Halfani Chusi**

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Tundu Lissu amesimulia alivyofuatiliwa hadi kupigwa risasi miaka mitano iliyopita.

Septemba 7, 2017, Lissu, akiwa Mbunge wa Singida Mashariki na Mnadhimu wa Kambi ya Upinzani Bungeni kipindi hicho, alishambuliwa kwa kupigwa risasi zaidi ya 38 mjini Dodoma.

Tukio hilo liliripotiwa kutendwa dhidi yake majira ya mchana, akishambuliwa kwa risasi akiwa anajiandaa kushuka kwenye gari lake nyumbani kwake Area D jijini Dodoma baada ya kushiriki mkutano wa asubuhi wa Bunge ambao pia alikuwa miongoni mwa waliochangia hoja.

Baada ya shambulio hilo, Lissu alipelekwa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Dodoma kupata matibabu ya awali na baadaye alipelekwa Nairobi, Kenya kwa ajili ya matibabu ya kibingwa kisha kuhamishiwa Ubelgiji ambako alitibiwa kwa muda mrefu zaidi na baadaye kuishi huko akihofia kurejea nchini kutokana na kile alichodai kukosa uhakika wa usalama wake.

Katika mahojiano na kituo cha runinga cha Clouds juzi alasiri, Lissu alifunguka kwa undani kuhusu tukio hilo lililotikisa kitaifa na kimataifa, akidai kulikuwa na magari mawili yaliyokuwa yanamfuatilia kuanzia alipotoka bungeni kwenda nyumbani kwa ajili ya kupata chakula cha mchana.

Lissu ambaye ni mtaalamu wa sheria, alisisitiza kuwa kuwapo kwake hai hadi leo ni Mungu tu na wala si utashi wake mwenyewe.

"Septemba 7 (2017), niliondoka nyumbani kwenda Dodoma, kuna eneo linaitwa Area D, kuna maghorofa mengi, ndiko wanakaa viongozi wa serikali na yanalindwa muda wote, nimeishi pale toka mwaka 2010.

"Nilifika bungeni, tukajadili na nilikuwa mtu wa mwisho kuzungumza katika ile session (kikao) ya asubuhi inayoisha saa saba mchana.

"Baada ya kumaliza, nikatoka nje nikampigia dereva wangu simu aje anichukue twende nyumbani tukale chakula cha mchana.

"Mimi siku zote ninakula nyumbani, ninapenda ugali na maziwa, ukiwa bungeni miaka ile njia rahisi ilikuwa inapita katikati ya uwanja wa ndege.

"Sasa siku hiyo ilikuwa imefungwa, sababu palikuwa panafanyiwa matengenezo. Kwa hiyo, ili uende Area D, inabidi uende mjini hivyo tukaelekea mjini," Lissu alisimulia.

Mwanasiasa huyo aliyerejea nchini mwezi uliopita baada ya kuwa ughaibuni kwa kipindi kirefu, alisema kuwa walipopita 'round about' ya Singida, wakapita 'round about' ya barabara ya Arusha ambayo inapakana na uwanja wa ndege, dereva wake alimwambia kuna magari mawili yalikuwa yanawafuata nyuma na walikuwa nayo tangu walipotoka mjini.

Lissu aliendelea kusimulia kuwa baada ya dereva wake kumwambia hivyo, alimjibu kwamba "hawa polisi wananifuatilia nini kwa sababu mimi nilikuwa ninasumbuliwa sana na polisi na nikiangalia wiki hii nimekaa kimya sana kwa sababu sijaongea jambo la kuwafanya wakose raha".

Mtaalamu huyo wa sheria aliendelea kusimulia kilichojiri, akitamka: "Tukafika Area C bado tuko nao, magari yalikuwa mawili -- Landcruiser nyeupe na Mitsubishi, tukaenda mpaka Area D tumekaribia getini kama kuna mtu anafahamu iliko Club84, kutoka hapo ni kama mita 20 hadi kufika hapo.

"Tulipopita pale, Landcruiser nyeupe ikapaki pembeni, Mitsubishi ikaja tukaingia nayo mpaka getini.

"Lile geti huwa linafungwa muda wote na huwa kuna walinzi wawili au watatu, lakini siku hiyo geti lilikuwa wazi na hakukuwa na mlinzi, tukapita tukaenda Block E niliyokuwa ninaishi."

Lissu alidai kuwa walipofika eneo hilo, waliingia sehemu ya kupaki gari huku lile gari lililokuwa linawafuatilia likiwa nyuma yao.

"Bahati nzuri siku hiyo magari yalikuwa mengi na nafasi ya kupaki ilikuwa imebaki ndogo yalikuwapo magari mengi ya viongozi wengine, yalikuwa bado hayajatoka. Kwa hiyo, sehemu ya kupaki ilikuwa moja. Kwa sababu sisi tulikuwa mbele, dereva akaiingiza gari kwenye nafasi iliyokuwa imebaki," alidai.

Lissu alidai kuwa dereva aliyekuwa anaendesha gari lililokuwa nyuma yao, alikuwa anatafuta eneo la kupaki na kwa kuwa hapakuwa na nafasi nyingine, alikosa nafasi, akageuza gari kuelekea walikotokea.

"Baada ya kuona hali hiyo, dereva akaniambia nisishuke kwanza nisubiri. Baada ya kuona sishuki kwenye lile gari na wao wakawa wananisubiri.

"Baada ya muda kidogo, mmoja aliyekuwa amekaa siti ya nyuma, akashuka akaenda kuongea mbele upande wa abiria, wakazungumza kidogo akarudi ndani.

"Ninafikiri walikuwa wanajadili 'sasa jamaa hashuki tunafanyaje?' Mimi hapo ninaona mchezo wote kwa kupitia vioo vya kwenye gari.

"Baada ya muda kidogo, yule aliyekuwa ameshuka na yule mwingine akafungua, wakiwa na mashine aina ya SMG (Short Machine Gun), hapo wakaachia.

"Paa! paaa! paaa! Walivyoanza tu, dereva wangu akanivuta upande wake, yeye akaruka akakimbia. Kwenye gari langu kuna friji nikawa nimelilalia na kiwiliwili changu nilikuwa kwenye siti ya dereva walinichakaza sana kwenye eneo la paja na mgongo kidogo.

"Walipomaliza kukawa kimya, ghafla baadaye dada yangu wa kazi, Amina ambaye huwa anatupikia chakula alikuwa anatusubiri twende kula, akaja akaona gari jinsi lilivyochakazwa.

"Na dereva wangu akatoka alikokuwa amejificha, mikono yangu ilikuwa imevunjwa na nimepigwa vibaya.

"Wakaninyanyua wakaniweka sawa kwenye siti. Baada ya hapo, wakanichukua kwa kutumia gari la Naibu Spika, wakanipeleka hospitalini," alisimulia.

Lissu alisema kuwa alimwambia dereva wake awapigie wafuasi wa chama chake kuwajulisha kilichotokea na alipofika hospitalini alimkuta Mwenyekiti (Freeman Mbowe) ameshafika baada ya kupata habari.

Alisema mwanzoni hakuona maumivu yoyote kwa kuwa mwili wake ulikuwa kama umekufa ganzi na baada ya hapo hakuelewa kilichoendelea kwa kuwa alipoteza fahamu na alizinduka akiwa Nairobi.

Hadi sasa hakuna aliyekamatwa na Jeshi la Polisi (lenye mamlaka hayo kisheria) kutokana na tukio la shambulio dhidi ya Lissu.

Lissu amerejea nchini kuendelea na shughuli za kisiasa, akitokea Ubelgiji alikokuwa anaishi.

Uamuzi huo umefanyika kwa baraka za chama siku chache baada ya Rais Samia Suluhu Hassan kuondoa zuio la mikutano ya kisiasa kwa vyama vya siasa lililodumu kwa takribani miaka saba.

FEBRUARI 5, 2023
Nipashe

# MAISHA

Baba, Mama na Mwana

*Jumapili*



Ukurasa 14


## Furahia chai ya masala

## MAISHA NI NYUMBA



Ukurasa 15

## Zingatia mpangilio mzuri wa nyumba yako




## KATUNIKA

Ukurasa 16




# VIPINI PUANI

Ukurasa 14


## MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA






| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| P | A | A | | U | D | A |
| U | | U | Z | A | | M |
| N | | | | N | | B |
| G | O | A | | A | K | U |
| U | | I | | | | L |
| Z | | T | O | A | | I |
| A | L | E | | O | G | A |


## FUMBO TOTO



Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyo wazi:

AYA, INI, ZNZ, AMA, BEI, UFA, ZUA, KWA, INZI, AU, KATA, ZAMBEZI, ZA, ATWANGA

## TOA TOFAUTI 5




## AMSHA AKILI

| | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 6 | 8 | 7 | 3 | 5 | 6 | 3 | 7 | 1 | 7 | 3 |
| 8 | 1 | 3 | 8 | 6 | 8 | 5 | 8 | 2 | 6 | 4 |
| 8 | 3 | 7 | 8 | 3 | 9 | 7 | 5 | 8 | 8 | 7 |
| 1 | 9 | 4 | 7 | 6 | 7 | 8 | 9 | 5 | 7 | 8 |
| 1 | 9 | 0 | 4 | 8 | 6 | 7 | 3 | 9 | 5 | 7 |
| 4 | 5 | 6 | 9 | 0 | 4 | 8 | 9 | 8 | 4 | 7 |
| 9 | 9 | 5 | 8 | 7 | 9 | 5 | 7 | 5 | 9 | 5 |




## WATOTO

# PAKA RANGI




## CHEKA

**Alichokifanya daktari**

JOHN alikwenda sokoni kununua nyanya na mambo yalikuwa hivi.

John: Nyanya zinauzwa kiasi gani?

Muuzaji: Kilo shilingi 1500

Kijana: Nimegizwa unisagie tunataka kwenda kula na chipsi nyumbani

Muuzaji: Kijana usitanie kazi za watu

Swali
Chaza inapatikana sehemu gani

## MAISHA NDIVYO YALIVYO

Na Flora Wingia



# Najuta kuzaa na wewe!

KARIBU tena msomaji wangu tuendeleze mada yetu ya wiki iliyopita. Bado tuko kwenye duru ya uhusiano kwa vijana. Nilijadili magumu yaliyomsibu dada mmoja ambaye umri wake unayoyoma bila kuona ndoa wala mtoto. Hajui afanyeje, anabakia kuduwaa.

Ni miongoni wa wadada wengi wanaopitia magumu wasijue chanzo chake. Akasema ana umri wa miaka 45 hajafurahia maisha ya kuwa na mume wala mtoto. Kila anayemchumbia humwachia njiani.

Nilitaja baadhi ya roho ambazo huenda ndizo zinazomfuatilia asione upenyo katika maisha yake. Roho mojawapo kuu ni ya kuchelewesha ambayo inazibeba roho zingine kadhaa. Nazo ni kukataliwa, kudharauliwa, roho ya mitala (kuoa wake wengi, kuoa na kuacha/kuachika) na roho ya mizimu.

Naam. Wakati wengine wanalilia ndoa wapitie mchakato wake, wengi wanatafuta mlango wa kutoka au walishabwaga manyanga na kuishi maisha yasiyo na masharti wala mikataba.

Upo msemo kwamba siri ya mtungi aijua kata. Usipoingia ndani ya nyumba huwezi kujua yaliyomo. Watu wengi huficha makucha wakiwa nje. Yaani ziko tabia ambazo huwezi kuziona kwa mtu wakati mnasaka uchumba. Zinajificha, mnaoana na hata kufikia hatua kupata watoto, ndipo wawili hao wanaanza kufahamiana vyema.

Siyo hicho tu, mbali na tabia za mtu zinazotokana na malezi alikolelewa hujitokeza, pia ziko roho zilizojificha kama hizo nilizotaja hapo juu zinaweza kusambaratisha ndoa iliyoanza vizuri na kuonekana ya mfano. Mapepo hayana huruma husubiri ufanikiwe ndipo yakupige!

Iko ndoa moja nilisimuliwa nakumbuka ambayo ilishavunjika kisheria mahakamani. Ilifungwa kwa sherehe kubwa na wawili hao wakabahatika kupata watoto watatu. Baada ya mtoto wa tatu kuzaliwa ndipo sarakasi zilianza.

Mwanamume akaanza tabia ya ulevi huku akimlazimisha mkewe kuambatana naye kulewa. Mkewe hakupenda sana tabia ya kulewa akawa anamkatalia. Matokeo yake mwanamume akawa anampiga kila mara jambo ambalo lilimkera sana.

Mwanamume huyu pia alikuwa hataki mkewe afanye kazi japokuwa ni msomi katika ngazi ya digrii masuala ya biashara. Vipigo, kung'atwa vilipozidi ndani ya miaka saba ya ndoa, akaamua kuondoka.

Kumbe wakati migogoro ikiendelea, mwanamume alikuwa na mchepuko huko nje kwenye viwanja vya pombe. Mke alipoondoka tu, akamleta nyumbani mchepuko huyo. Watoto akawapeleka kwa wazazi wake Kilimanjaro wakasome huko.

Mwanamume huyu wakati anaishi na mkewe wa ndoa, aliwahi kumtamkia kwamba "najuta kuzaa na wewe". Haya ni maneno mabaya sana kutamkwa na mwanadamu. Hiyo ina maana kwamba hata hao watoto umewakataa.

Athari za matamshi haya jamaa atazikuta huko mbele. Watoto ni baraka kwa Mungu. Unapojuta kupewa watoto hao kupitia mkeo kuwazaa, unamkufuru Mungu aliyekupa neema na baraka hiyo! Huo ndio ukweli!

Watoto hao watakapokuja kumkataa baba huyo hapo baadaye asitafute mchawi, kwa kuwa yeye ni mhusika mkuu kwa maneno ya kinywa chake mwenyewe. Lipo andiko la Mungu linasema, "amekamatwa kwa maneno ya kinywa chake, amefungwa kwa maneno ya kinywa chake".

Hata hivyo, jamaa huyu baada ya kumfurahia mchepuko wake, akaamua kwenda mahakamani kuomba watengane, jambo ambalo mkewe wa ndoa aliridhia, hivyo kila mtu kuwa huru na mambo yake. Mahakama ilipitisha hukumu huku ikiruhusu mama kuwaona watoto wake wakati wowote na hata kuwa nao.

Maisha Ndivyo Yalivyo. Wakati wengine wanatafuta kuolewa au kuoa, wengine wanatafuta kuachana baada ya kubarikiwa kupata ndoa nzuri zilizojaa chereko chereko!

Hata hiyo, uzoefu katika duru la mahusiano katika ngazi ya ndoa unaonyesha, wengi walioachana kibabe hawakuishi maisha ya amani zaidi ya kuugulia maumivu ya ndoa.

Kwa mfano, mwanaume anayeacha mkewe kibabe na kuoa mwingine haraka, baada ya muda hugeuka nyuma na kujilaumu kwa uamuzi ule. Wengi hujutia uamuzi. Pengine walihitaji subira na ushauri tu.

Lakini wengine inabidi waamue hivyo kutokana na tabia alizokuwa nazo mkewe. Huenda alikuwa na tabia za kihuni, muongo, siyo mwaminifu na kadhalika.

Hizo na zingine ndizo tabia nilizodokeza awali kwamba huwa zimejificha ndani ya mtu pale mwanzoni. Zikiibuka baadaye ndipo mtikisiko unatokea kwenye ndoa nyingi.

***Mpenzi msomaji, bila shaka umejifunza m hapo kuhusu mikikimikiki ndani ya ndoa. Tukutane wiki ijayo. Je, una kisa? Ujumbe mfupi 0715268581.***

## WARAKA WA NDANI

Na Godfrey Mushi



# Hesabu gharama kabla ya kuingia kwenye ugomvi

Moja ya hasara kubwa ya kufarakana, ni kunyang'anywa utu na uwezo wa kupima gharama za hasara. Usianzishe vita kabla ya kupima gharama kwa vile hata wanadiplomasia wengi duniani, wanaamini kwamba kufuata njia ya amani kuna faida kubwa.

Kufarakana huvuruga aina zote za mafanikio, maendeleo na kufunga milango yote ya baraka. Kama ni ugomvi kwenye familia au kwenye jamii ama kwenye taasisi, basi hata taratibu za kistaarabu za kuishi nazo hutikiswa.

Katika siku za usoni, kumekuwapo na mijadala katika mitandao ya kijamii, ikihusu sakata la ndoa ya mtaalam wa tiba mbadala, Dk. Juma Mwaka na mwenza wake, Queen Masanja.

Januari 25, mwaka huu, kulinukuliwa katika baadhi ya vyombo vya habari, juu ya taarifa za kuvunjwa kwa ndoa ya mtaalamu huyo, baada ya mwenza wake kudaiwa kuomba talaka.

Baada ya uamuzi huo kufanyika, kumetokea mitazamo tofauti baina ya wanazuoni wa Kiislamu, hivyo kusababisha Baraza la Ulamaa ambalo ni chombo muhimu katika Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA), kuingilia kati na kuweka mizania sawa. Ndivyo inavyotakiwa kwa taasisi kulinda heshima yake ili isiporomoke. Haya yanayojitokeza sasa kwa wenzetu wenye ndoa yao, yatufunze sote tulioko kwenye ndoa, kuhesabu gharama kabla ya kugombana.

Baraza la Ulamaa katika kikao chake kilichofanyika Februari 1 na 2, mwaka huu, chini ya Mwenyekiti wake, Mufti na Shehe Mkuu wa Tanzania, Dk. Abubakar Zubeir bin Ally, lilitengua uteuzi wa Shehe wa Mkoa wa Dar es Salaam, Alhad Mussa Salum, kuanzia Februari 2, 2023.

Uamuzi wa kumtengua Shehe Alhad, umekuja ikiwa imepita wiki moja tangu, kiongozi huyo kudaiwa kutangaza kuivunja ndoa hiyo ya mtaalamu wa tiba mbadala kutokana na ombi la mwanamke huyo kudai talaka. Hata hivyo, siku mbili baadaye, yaani Januari 27, Baraza la Ulamaa lilikutana kwa dharura na kubatilisha uamuzi huo.

Ndoa hiyo ilivunjwa baada ya kikao cha Kamati ya Mashehe wa Mkoa wa Dar es Salaam, chini ya uenyekiti wa Shehe Alhad Mussa Salum, kuketi kwa dharura na kuridhia maombi ya Queen kutaka apewe talaka.

Hakuna shaka kwamba, mambo mengi yanayobishaniwa juu ya sakata hilo, yana nafasi kubwa ya kutafsiriwa katika Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971 (Law of Marriage Act, Cap. 29) ambayo inaelekeza vyema juu ya kuzingatiwa kwa kanuni za mashauri ya ndoa, kanuni za mabaraza ya usuluhishi wa ndoa na kanuni za ndoa kuhusu kazi za manaibu wasajili wakuu wa ndoa na talaka.

Ukiiacha taasisi kama BAKWATA, ambayo yenyewe imepewa mamlaka ya kusikiliza na kusuluhisha migogoro ya ndoa za watu wa Jumuiya ya Kiislamu, kupitia chombo chake, ambacho ni Mahakama ya Kadhi; ieleweke kuwa ni mahakama pekee, ndiyo yenye mamlaka ya kuvunja ndoa pale inapojiridhisha kwamba kuna sababu ya msingi kufanya hivyo.

Kwa muktadha wa kisheria, ndoa imetafsiriwa kama uhusiano wa hiari kati ya mwanamume na mwanamke, kwa muda wa maisha yao yote, hivyo, kusuluhisha migogoro ya wanandoa ni muhimu zaidi ili lengo la ndoa litimie la wanandoa kuwa na uhusiano wa hiari kwa muda wote wa maisha yao.

Watanzania wengi wangependa kuona ndoa zao zinakwepa mitego ya kutumbukia katika migogoro, kwa ustawi wa jamii, taifa na familia husika. Talaka iwe ni hatua ya mwisho ya utatuzi wa migogoro, baada ya wanandoa kupata fursa ya usuluhishi.

Ni nani mwenye uwezo wa kudai talaka, kati ya mume au mke? Jibu ni kwamba mume au mke, anaweza kuomba talaka iwapo amefanyiwa mambo au jambo ambalo ni kinyume cha matakwa ya sheria ya ndoa.


Hakuna mshindi katika kufarakana. Mafarakano huzaa hasara. Liwe somo kwa kila mmoja wetu kujifunza kuhesabu hasara, kabla ya kugombana.

Godfrey Mushi ni Mwandishi Mwandamizi wa Gazeti la Nipashe, Kanda ya Kaskazini
***anapatikana kwa barua pepe:ghandsome79@gmail.com***
***Simu ya mkononi: +255 767 535490***

# HARUSI







JANUARI 27, MWAKA HUU NI SIKU YA KUKUMBUKWA KWA WANANDOA BIKELA NA ZAWADI KHERI, BAADA YA KUFUNGA PINGU ZA MAISHA KATIKA MASJID TWALHA, ILIYOKO MBURAHATI, KISHA WALIANDALIWA SHEREHE ZA AINA YAKE KATIKA UKUMBI WA SIMBA OIL JIJINI DAR ES SALAAM.





# MITINDO

## EPUKA MAKOSA

INAPOFIKA mwishoni mwa wiki, watu wengi wanapenda kutoka na familia zao kwa lengo la kwenda kukutana na ndugu na jamaa au kwenda katika maeneo ya starehe.

Hata hivyo, uchaguzi wa mavazi ni jambo la kuzingatia ili kukupa uhakika utatokaje katika kipindi hicho.

Hata hivyo kuna baadhi ya vitu vitanakiwa kuepukwa ambavyo wengi hawazingatii na kujikuta wakionekana vibaya.

**Vaa kulingana na mazingira**

Hakikisha unavaa nguo kulingana na mazingira unayokwenda. Epuka kuvaa nguo zitakazofanya kuwa tofauti na sehemu unayokwenda.

Kwa mfano epuka kuvaa jezi za timu za mpira unapotaka kwenda sherehe

Masharti ya kuchomekea

Marufuku kuvaa mashati yaliyozidi ukubwa, kama lipo sawa epuka kuvaa mlegezo, mkanda mrefu.

**Hakikisha una suruali nyeusi**

Kila mtu anajua umuhimu wa suruali nyeusi kuwa nayo. Nguo hii inapendeza kuvaa na nyingine bila wasiwasi.

**Saa**

Kama umevaa suruali ya jeans au kadet, unaruhusiwa kuvaa saa ya aina yoyote.

lakini kwa vazi la suti au suruali ya kitambaa, epuka kuvaa saa na mkanda wa plastiki.







UREMBO

Na Mary Geofrey



# VIPINI PUANI

## Urembo unaong'arisha lakini....

MIAKA ya nyuma ilizoeleka wanawake pekee ndo wanastaili kuvaa vipini puani na hata wengine waliweka kipini zaidi ya kimoja.

Katika mtindo wa kale, kipini kilikuwa kinawekwa katika pua moja na hakika mtu alipendeza hasa kutokana na aina ya kipini alichokuwa nacho.

Lakini siku hizi imekua tofauti kidogo, wanaume pia wameanza kutumia urembo huu wa vipini puani japokuwa inaonekana kwenda kinyume na maadili ya Tanzania.

Kutokana na mabadiliko ya mitindo ya maisha, kwa saa uvaaji wa vipini kwa wanawake umekuwa tofauti, kwani mitindo ya kutoboa pua zote na kupambwa na vipini umezidi kusambaa na kuonekana kama jambo la kawaida.

Kuna baadhi wanasema kwamba urembo huo unaleta mwonekano mzuri zaidi.

Hata hivyo, aina hii ya uvaaji vipini ni jambo gumu kufanywa na wanaume, hata kama unapenda aina hii ya urembo ni lazima kujitafakari kwa kuwa ni kinyume na maadili ya Kiafrika.



MAPISHI

Na Mary Geofrey

# Furahia chai ya masala



MASALA ni mkusanyiko wa viungo tofauti pamoja na maziwa kwa ajili ya kuweka ladha na harufu nzuri kwenye chai, kahawa au chakula chochote.

Idadi ya viungo vinaweza kutofautiana, kwa sababu hakuna mchanganyiko kamili uliowekwa, lakini kuna viungo vikuu vya asili vinavyotumiwa.

Asili ya viungo vya joto vinaongezwa kwenye chai ya masala kwa mfano, kadiamu, tangawizi, mdalasini, karafuu, pilipili nyeusi, mbegu za shamari.

Namna ya kuchanganya viungo

Unaweza pia kutumia tangawizi safi badala ya tangawizi kavu.

Viungo vingine vinavyowezekana kwa chai ya masala inaweza kujumuisha 'nutmeg', mzizi wa licorice, zafarani, almond na maua ya maua.

Unaweza pia kubadilisha viungo vyovyote unavyopenda, kwa mfano, tumia nutmeg badala ya karafuu na zafarani badala ya mdalasini.

Seti ya manukato kwa chai ya masala inaweza kutayarishwa au kwa kujitegemea ukavisaga na kuwa unga au kununuliwa katika duka maalum kwa njia ya unga.

Namna ya kupika chai

Unaweza kuchemsha maji au maziwa, baada ya hapo ukaweka unga wako wa viungo na chai yako itakuwa tayari.

## MAISHA NI NYUMBA

**Na Elizabeth Zaya**



# Zingatia mpangilio mzuri wa nyumba yako

MPANGILIO wa ndani ya nyumba unagusa vitu na maeneo mengi. Unapokuwa na mifumo ambayo umejiwekea bila shaka itakusaidia kuwa na nyumba nadhifu, safi yenye mpangilio na hivyo kurahisisha maisha.

Hapa nataka tuangalie vitu na maeneo mbalimbali ya nyumbani yanayohitaji kuwa na mpangilio mzuri na jinsi ya kuwa na mfumo wa kuwezesha kufanikisha kuipendezesha na kuiweka imara.

Katika mpangilio wa nyumba miongoni mwa vitu ambavyo vinapaswa kuepukwa ni pamoja na kutotunza vitu vilivyotumika.

Naweza kusema kwamba hii ni aina mojawapo inayochangia nyumba ionekane chafu na hata kupoteza mvuto wake hata kama ni nzuri.

Kupangilia unaweza kuanza mahali popote, sebuleni, chumba cha kulala, jikoni, sehemu ya chakula au vinginevyo kulingana na unavyoona wewe.

Kwa kuanza na sebule, hakikisha unapasafisha kila siku, panga kila kitu katika nafasi yake na epuka kuacha vitu vimedondoka hovyo iwe karatasi, nguo na uondoe vyote visivyostahili kuwapo eneo hilo la sebule.

Kwa upande wa jikoni, nafahamu kwamba katika baadhi ya nyumba, jikoni ndilo hutumika kama njia kuu ya kupita kuingilia vyumba vya ndani ambapo hata wageni hutumia njia hiyo kuingia sebuleni.

Kama jiko ndiyo njia kuu, uwapo wa vifaa vingi, vyombo, vifaa vingine vilivyowekwa ovyo pasipo na mpangilio mzuri kunaweza kuharibu mwonekano wa nyumba yako.

Na hata kama si njia ya kuingilia ndani, hakikisha napo pamepangiliwa ipasavyo. Usitunze vyombo vichafu humo. Unapovitumia vioshe na kuvipanga katika eneo vinapopaswa kuwekwa.

Safisha majiko yako unayotumia na hata sakafu na kupangilia vizuri kila kitu jikoni kikae sehemu yake.


Katika eneo linalotumika kwa chakula, napo paweke vizuri pavutie, pasikae vitu vingi ovyo ovyo. Si vibaya ukaweka hata kaua pekee katikati ya meza kunogesha.

Kwenye chumba cha kulala, tandika kitanda vizuri na weka mito yako kwa mpangilio wa kiubunifu kunogesha.Bila kusahau meza yako ya kujirembea kupanga vipodozi vyako kwa uzuri baada ya kujiremba na eneo la kuwekea nguo, viatu na vitu vinginevyo.

Unapaswa kuweka ndani ya kabati vitu unavyohitaji huku ukipanga vile unavyotumia mara kwa mara maeneo ya karibu na vile unavyotumia mara chache maeneo ya juu.

Kadhalika, kama una watoto wadogo, midoli inaweza kuwa ni moja ya vitu vinavyokupa changamoto kubwa ya kuweka kwenye mpangilio nyumba yako. Midoli inaweza kusambaa kila mahali hata ikafikia hatua ya kuumiza watu, ili kuepukana na hilo, ni vema ukaandaa kifaa maalumu cha kuhifadhia kama vile vitenga vikubwa kwa vidogo kwenye vyumba vyote vya watoto pamoja na maeneo yao ya kuchezea.

Au kutengeneza shelfu za wazi ukutani ili wanapomaliza wanahifadhi humo.





## Namna ya kugawa chumba kwa mbao

**Na Restuta James**

WAKATI mwingine vyumba au sebule inahitaji kugawanywa kwa kusudi maalum. Kufanya hivi imerahisishwa sana, na kimsingi sio jambo gumu tena.

Kuna mbinu bora na za kisasa za kugawanya vyumba ambazo zinaleta mwonekano maridhawa.

Huhitaji tena fundi ujenzi, mchanga au kutimua vumbi ndani ya nyumba ili ugawe chumba. Unahitaji tu fundi seremela mbunifu ili aweze kujua atumie nini kuboresha mwonekano wa nyumba au chumba chako.

Kama inavyoonekana pichani, aina hii ya kugawa chumba inaongeza nakshi na hivyo kuifanya nyumba yako iwe sehemu nzuri ya utulivu yenye kukupa faraja.

Wataalam wa mapambo ya ndani wanaeleza kuwa unaweza kutumia mbao ngumu au hata zile laini kwa kuziongezea nakshi ya maua au kuzing'arisha kwa polishi.

Wanaeleza kuwa sio lazima ubadili mwonekano wa nyumba yako pale unapohitaji kuigawa tu, unaweza kubadili hata mwonekano wa kuta kwa kutumia njia hiyo.


Mathalani, ukuta wa kwenye korido unaweza ukaweka nakshi ya ubao iliyopolishiwa vyema na ikabadili mwonekano.

Kwenye veranda pia, unaweza kutengeneza mazingira ya 'binafsi' kukupa raha kwa kutumia aina hiyo ya ugawaji na ukaendelea kufurahia madhari ya nyumba yako.

Wataalam hao wanaeleza zaidi kwamba mbali ya nyumba, unaweza kubadili mwonekano wa bustani yako kwa kuigawa kwa mbao au mapambo yatokanano na mbao laini.

Kwa mujibu wa wataalam hao, hii ni njia ya kisasa kabisa ya kunakshi nyumba. Njia hii inatajwa kuwa nafuu zaidi kuliko matofali, rahisi na ya haraka.

# KATUNI




*KINYUNYIZO CHA LEO... ...FUNUA KOMBE MWANAHARAMU AUMBUKE...

# Viongozi EAC wajadili mapigano DRC

**BUJUMBURA,** BURUNDI

VIONGOZI wa mataifa ya Jumuiya ya Afrika Mashariki wanakutana nchini Burundi, kujadili mapigano yanayoendelea mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo. Mkutano huo unafanyika siku moja baada ya Papa Francis kutoa wito wa kusitishwa mapigano wakati akikamilisha ziara yake ya siku tatu nchini humo.

Mapigano yameendelea kushuhudiwa hata wakati wa ziara ya kiongozi huyo wa kanisa katoliki duniani ikifanyika nchini humo.

Watu kadhaa waliripotiwa kuawa katika siku chache zilizopita katika mapigano kati ya vikosi vya serikali na makundi ya waasi.

Mkutano huo wa viongozi wakuu wa serikali unafanyika wakati mapigano yanaendelea Kivu ya kaskazini.

Waasi wa M23 wanaotuhumiwa kuhusika na ghasia hizo hivi karibuni wamedhibiti miji kadhaa.

Kundi hilo linashutumiwa kwa kukiuka makubaliano ya kusitisha mapigano yaliyonuiwa kutoa fursa ya mazungumzo ya kusitisha ghasia hizo.

Wasiwasi unaongezeka kati ya Congo na jirani yake Rwanda, hali hiyo pia itajadiliwa katika kikao cha viongozi hao wa kanda.

Jumuiya ya Afrika mashariki imetuma wanajeshi ndani ya DRC kuvisadia vikosi vya serikali na walinda amani wa Umoja wa mataifa kupambana na makundi kadhaa yaliojihami kwa silaha.

Mamia ya watu wameuawa na wengine zaidi ya laki nne wametoroka makazi yao kufuatia mapigano katika eneo hilo lenye utajiri wa madini.

**BBC**



Papa Francis akiwasili katika uwanja wa ndege wa Juba nchini Sudan Kusini, kuanza ziara ya siku tatu inayolenga kuendeleza amani na maridhiano katika nchi hiyo. **PICHA: AFP**

# Puto la ujasusi linazidi kuleta mvutano mkali Marekani, China

**WASHINGTON,** MAREKANI

CHINA imetoa wito wa kutumika busara kushughulikia mzozo kuhusu uwepo wa puto linalodaiwa la nchi hiyo ambalo linapaa angani kuelekea mashariki mwa Marekani.

Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani, Antony Blinken, alilazimika kukatisha ziara yake nchini China, akisema kuwepo kwa puto hilo linalodaiwa kuwa la kijasusi ni kitendo cha kutowajibika.

Hata hivyo, Marekani iliripoti kuonekana kwa puto lingine la pili linaloelea katika anga la Amerika ya Kusini.

China ilielezea masikitiko yake juu ya puto hilo kwenye anga ya Amerika, ikisema kutokana na hali ya hewa lilipoteza mwelekeo.

Mara ya mwisho puto hilo lilionekana eneo la Missouri, na linatarajiwa kufikia pwani ya mashariki ya Amerika karibu na Carolinas mwishoni mwa wiki hii.

Marekani imeamua kutoliangusha puto lolote kukwepa hatari yoyote ya vilivyomo ndani ya puto.

Tukio hilo linakuja huku kukiwa na mvutano kati ya Marekani na China.

**BBC**

# Macron, Netanyahu wateta kuhusu Iran

**PARIS,** UFARANSA

RAIS wa Ufaransa, Emmanuel Macron na Waziri Mkuu wa Israel, Benjamin Netanyahu, wamejadili mpango wa nyuklia wa Iran na vita vinavyoendelea kati ya Russia na Ukraine.

Taarifa iliyotolewa jana jioni, na Ikulu ya Elysee mjini Paris, ilisema kuwa kwenye mazungumzo ya viongozi hao wawili, Macron alitilia mkazo haja ya kuchukuwa hatua madhubuti kwenye suala la programu ya nyuklia ya Iran.

Rais huyo wa Ufaransa pia alilalamikia kile alichokiita ukosefu wa uwazi wa Iran katika mazungumzo yake na Shirika la Nishati ya Atomiki la Umoja wa Mataifa (IAEA).

Netanyahu na Macron kwa pamoja walielezea wasiwasi wao juu ya kile wanachosema ni vitendo vya kuondosha utulivu kwenye eneo la Mashariki ya Kati na Ghuba ya Uajemi, kwa mujibu wa vyanzo vilivyozungumza na shirika la habari la Ujerumani (dpa).

Kuhusiana na uvamizi wa Rusia nchini Ukraine, taarifa ya serikali ya Ufaransa ilisema Macron aliitaja hatua ya Iran kuunga mkono uvamizi huo kuwa inazidi kuiweka kwenye hatari ya vikwazo na kutengwa.

Upande wa Israel ulisema viongozi hao wawili walijadiliana njia za kukikabili kitisho cha nyuklia cha Iran kwa upana, Netanyahu alitoa wito wa kuuwekea vikwazo utawala wa Iran.

Mazungumzo hayo yalifanyika wakati hali ya wasiwasi ikiongezeka kati ya Israel na Palestina, huku Macron akimhakikishia Netanyahu mshikamano wa nchi yake na Israel.

Hata hivyo, Macron alielezea umuhimu wa kuepuka hatua zinazoweza kuchochea muendelezo wa machafuko ambayo tayari yamepoteza maisha ya raia wasio na hatia kwa pande zote mbili.

**DW**

## MAKALA

# KUFAULU MTIHANI NI KUFAULU MAISHA?



Na Magabilo Masambu

**Unakuta mtu ni mtumishi wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kwa mfano, mshahara wake wa kawaida sana lakini mali na fedha anazomiliki ni nyingi. Watu wa pembeni ambao hawajui kama pengine hizo pesa zinatokana na rushwa, wanaamini kuwa ukifanya kazi TRA, basi utakuwa tajiri haraka maana wanalipa vizuri.**

ELIMU ni ufunguo wa maisha kama wasemavyo waswahili. Dhana ya elimu ni pana, viwango vya elimu vinatofautiana na aina za elimu pia ni tofauti. Dhana tuliyo nayo wengi tukizungumza juu ya elimu, tunamaanisha mwanafunzi atoke darasa la kwanza mpaka chuo kikuu.

Kwa maana nyingine, mtu atajiona anayo elimu ikiwa tu atakuwa amepita katika nyanja zote hizo za elimu. Kabla ya mfumo wetu haujabadilika tulipotekeleza kwa kiasi elimu ya kujitegemea nyakati za ujamaa, elimu ilikusudiwa katika kila hatua anayomaliza mhitimu, angalau awe na ujuzi wa jambo lolote la kufanya. Kama ni elimu ya kilimo katika ngazi ya chini kabisa, basi awe na uwezo fulani wa kutoa matokeo ya jambo alilojifunza.

Baadaye, mtazamo wetu katika elimu ukabadilika, sasa ukawa juu ya elimu kuandaa wanafunzi ili kuendelea na hatua za juu zaidi za elimu, nikiwa na maana kwamba darasa la saba aandaliwe kuingia kidato cha kwanza na si kuandaliwa kufahamu ujuzi kwa hatua hiyo. Kidato cha nne kuandaliwa kwenda kidato cha sita na wa kidato cha sita afike chuo kikuu. Malengo na mtazamo wetu kama taifa ukawa hivyo.

Ushahidi wa hili unaweza kuona mtu aliyemaliza kidato cha sita anaweza kufanya kazi gani kama sehemu ya ujuzi? Badala ya kujifunza maarifa na ujuzi, tukajifunza zaidi kuhusu ustaarabu na kwamba sisi ni wasomi na baadhi ya kazi si zetu bali za watu ambao hawajasoma. Tukikwambia unaweza kutengeneza nini, huna zaidi ya kuzungumza Kiingereza kizuri kama ulibahatika kukifahamu au kufanya hesabu ambazo nazo kwa maisha ya kawaida, haziwezi kukusaidia sana. Kama utakuwa umeishia kidato cha sita, mfano hesabu za 'Calculus' utazifanyia nini?

Matumaini tuliyo nayo wengi wetu ni kuamini kwamba ukishafaulu mitihani yako ya ngazi yoyote umetoboa maisha. Ni kweli kwamba elimu ni muhimu na kupitia elimu hii ninayoimaanisha, wengi wamefanikiwa na ikiwa wengi wangelifanya kazi kwa uaminifu mkubwa bila kuiba fedha za mashirika au za umma, bado mafanikio ya elimu zao yangesalia historia kwa kuwa anayekuajiri hawezi kukulipa mshahara utakaokuwa mkubwa kuliko kile anachopata yeye. Akifanya hivyo, kwanza hataweza kuendelea kukulipa maana utamfilisi. Lakini pili hutamtumikia maana una pesa kuliko yeye. Kwa maana hiyo, mwajiri yeyote anakupatia fedha kiasi ambacho kitakuwa kinakutosha kula na kufanya matumizi madogo madogo ili uendelee kumtumikia maisha yako yote.

Tunapokuwa kwenye taasisi za elimu tukipata masomo yetu tunakuwa na matumaini makubwa sana juu ya mafanikio yatakayotokana na elimu lakini uhalisia uko kazini japo wengi wanaofanya kazi tayari huwa hawawezi kusema ukweli juu ya mishahara yao. Unakuta mtu ni mtumishi wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kwa mfano, mshahara wake wa kawaida sana lakini mali na fedha anazomiliki ni nyingi. Watu wa pembeni ambao hawajui kama pengine hizo pesa zinatokana na rushwa, wanaamini kuwa ukifanya kazi TRA, basi utakuwa tajiri haraka maana wanalipa vizuri.

Lakini kama tunataka kufanikiwa ni muhimu kubadili mawazo na mtazamo wetu. Mtazamo wetu uwe juu ya kuitumia elimu yoyote, iwe ya biashara umejifunza kwa mtu, iwe ni ya ufundi umejifunzia nyumbani, iwe ya ujuzi uliyojifunzia shuleni na kadhalika. Tuondoe mawazo kwamba ili kutoboa maisha lazima tuwe tumefaulu masomo yetu katika mfumo rasmi. Tukifanya hivyo tunaweza kuchelewa kufanikiwa.

Jambo la pili, tuachane na kasumba ya kudhani kwamba tuliofika vyuo vikuu hatustahili kufanya kazi fulani kwa sababu ya elimu zetu. Kuna kazi wanafanya wazazi wako na kazi hiyo ndiyo iliyotoa ada ya kukusomeshea lakini eti ukishamaliza elimu yako ya chuo kikuu, unaiona kazi hiyo ni ya kishamba kwa sababu tu haifanani na ulichosoma!

Ujinga tulio nao siku hizi, ikitokea mtu mwenye digrii au 'mastazi' akaonekana mathalani anachoma mishkaki, basi eti hiyo ni habari kubwa mjini na vyombo vya habari vinajaa kutaka kufahamu kwa nini una digrii lakini unachoma mishikaki. Huwa najiuliza ni mahali gani pameandikwa kwamba hawa ndio wanastahili kuchoma mishkaki? Kwanza digrii ilikuwa zamani nyakati ambazo hata joho lilikuwa na heshima kwenye jamii maana siku hizi yamegeuka kuwa magauni kwa sababu sasa yanavaliwa na kila mtu.

Kwa hiyo ninachotaka kusema ni kwamba suala la kufaulu mitihani ni muhimu lakini haiwezi kuwa hakikisho kwamba ukishafaulu na kufika chuo kikuu utatoboa. Lakini pia kama mawazo yetu yatakuwa kwamba tunataka kufanikiwa kupitia elimu zetu basi kwa vyovyote vile tutakuwa wezi, mafisadi na wahujumu uchumi na malengo ya elimu katika nchi kupotea kabisa, ambayo mojawapo ni kutoa huduma kwa jamii badala yake tutazifanyia biashara elimu zetu.

Mwisho, kwa yule ambaye hakupata fursa ya kuendelea na masomo ya ngazi ya juu, ndio muda muafaka wa kutazama fursa iliyoko mbele yako ili rafiki yako atakapotumia miaka 10 kumaliza shule, akitoka huko unamwajiri maana utakuwa muda wa kutosha kujijenga vizuri. Maisha huwa ni mlinganyo pambana na zaidi wasomi wengi wameajiriwa kwenye kampuni za watu waliopata elimu kidogo tu ambao walitumia muda wao vizuri.

**0689157789**
**magabilomjalifu@gmail.com**
**DAR ES SALAAM-TANZANIA**

## BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# *Siwalaumu wakwe, nailaumu roho yangu kwa kumpenda binti yenu*



Na Adam Fungamwango

MAMBO yanabadilika kizazi hadi kizazi, kwani ni aghalabu sana miaka ya zamani kijana au binti akitaka kupata mchumba lazima wazazi wahusike.

Kwanza kabisa wazazi walikuwa na wajibu wa kumtafutia kijana au binti wao mchumba ambaye wao wataona anafaa kwa vigezo wanavyovifahamu wenyewe.

Pili kijana au binti anaweza kumpata mchumba, lakini ni lazima kwanza ampeleke kwa wazazi wake wakamthaminishe kabla ya kukubali kuwa huyu ni mtu sahihi wa kuoa.

Wazee wa zamani walikuwa na vigezo vingi sana, vingine ni muhimu sana hata kwenye maisha ya leo, lakini vipo ambavyo kwa sasa vimepitwa na wakati.

Vigezo vya binti kutwanga sana, au kijana kulima sana, au ametoka kwenye familia masikini kwa sasa vimepitwa na wakati. Kuna vigezo muhimu ambavyo hadi leo bado ni muhimu ambavyo ni tabia njema, adabu na heshima, uwezo wa kujituma kwa ajili ya kutunza mke au mume. Kwa kuongeza tu, wazee wa zamani walikwenda mbali sana wakawa hadi wanaangalia ukoo wa kijana au binti ambaye mtoto wao anataka kwenda kuchumbia au kuchumbiwa.

Kukiwa na mtu mmoja tu kwenye familia hiyo ana magonjwa ya kuambukiza au ya kuzaliwa nayo, ilikuwa ni kigezo cha kumkataza na kuukataa uchumba huo.

Si hivyo tu, hata ulevi wa kupindukia, ugomvi wa mara kwa mara wa familia husika, uliweza kumfanya mmoja kati ya wanandugu kukosa mchumba.

"Unakwenda kuoa pale mwanangu, hapana, yule kaka yao ni mlevi sana, anaweza kuwaambukiza wajukuu zangu. Wazazi wao wanagombana kila kukicha, na wewe usije ukaingia kwenye janga hili mwanangu." Wazazi walikuwa wanawatahadharisha watoto wao.

Kwa bahati nzuri, vijana zamani kwa asilimia 90 walikuwa wakiwasikiliza zaidi wazazi wao, walikuwa wakikubaliana nao.

Mzazi akisema huyu kijana, au binti simtaki, ujue imetoka hiyo, hakuna mjadala.

Kwa sasa si hivyo tena. Wazazi wamekuwa wakipelekewa tu ili wawaone na si kuwathaminisha tena. Hakuna kinachobadilika. Wazazi sasa hawana tena sauti kwa vijana wao, kwani kizazi hiki chenyewe kinataka uhuru wa kuchagua kile wanachokipenda bila kuingiliwa. Ni vema kabisa. Hili si jambo baya kwa sababu mwisho wa siku aliyemchagua ndiye anayeishi naye. Nimesema hata wazazi walipokuwa wanawachagulia watoto wachumba, au kuwathaminisha kabla hawajawaoa, kuna faida na hasara zake. Na hata sasa ambapo watoto wameachiwa wenyewe uhuru pia kuna faida na hasara zake.

Faida ni kwamba kijana anamchagua mtu ambaye anampenda moja kwa moja kwenye nafsi yake na si yule ambaye ameletewa au kuambiwa akamuoe.

Hasara inakuja pale inapotokea, mtu uliyempenda kumbe ana matatizo mengi ya kinidhamu na kimaadili ambayo hayakuonekana awali, lakini yamekuja kuonekana baadaye ndani ya ndoa.

Hapo sasa hata wazazi wanashindwa wasaidie vipi kwa sababu hawakuhusika kwa lolote, badala yake wameambiwa tu na kutaarifiwa harusi.

Wanamuziki wa zamani hawakukaa kimya kwenye hili. Maximillian Bushoke, akiwa na bendi ya DDC Mlimani Park Orchestra alitunga wimbo aliouita 'Siwalaumu Wakwe'. Kwa mujibu wake kilikuwa ni kisa cha kweli kilichomtokea yeye mwenyewe jijini Dar es Salaam mwanzoni mwa miaka ya 1980, na kilirekodiwa mwishoni mwa miaka hiyo.

Ni kwamba alimpenda binti tajiri kiasi kwamba msichana akampeleka kumtambulisha kwa wazazi wake. Kilichotokea huko ni balaa. Wakwe walimdhalilisha na kumwambia hawawezi kuwa na mkwe kama yeye. Kwanza fukara, halafu kazi yenyewe anayoifanya ya muziki haiwezi kumfanya binti yao awe na furaha. Kama nilivyosema awali zamani wazazi wakisema, basi ni amri. Kila kitu kikaishia hapo hapo. Bushoke kwa sababu ni mwanamuziki hakuliacha hivi hivi, akaandika mashairi ambayo ukageuka wimbo maarufu hata leo.

"Sioni raha ya dunia, roho inaninyong'onyea, naomba fikra zikitoke nisipatwe na mfadhaiko wa akili mama, kwa mawazo. Kuwa fukara mimi sikupenda kwa nini iwe sababu nikakataliwa nisimuoe binti tajiri, ama kweli ufukara jeraha la ulimwengu.

"Fukara lake jasho daima. Kwa kauli yangu ya ukiwa siwalaumu enyi wakwe, ninailaumu roho yangu kwa kumpenda binti tajiri, nabaki na majonzi moyoni, najisikitikia."

Angalia vijana wenye heshima na adabu. Pamoja na kudhalilishwa, hawalaumu wazaa chema. Anailaumu roho yake mwenyewe kwa kumpenda binti yao. Ni maneno ya hekima na busara kutoka kwa kijana huyo wa enzi hizo.

Sipati picha kwa kijana wa sasa afanyiwe kitu kama hicho, halafu aambiwe atunge mashairi ya bongo fleva kutokana na kisa hicho.

Nina uhakika hao wakwe watanangwa hao, watakashifiwa kuwa hawana lolote. Binti huyo pamoja na kwamba hana kosa, anaweza kuwaambia wakwe kwanza binti yenu hana lolote huyo. Lakini kijana huyo yeye alibaki akijisikitikia mwenyewe bila kuzua mgogoro au maneno kwenye familia ya mchumba wake, ili binti aendelee kuishi vema na wazazi wake.

# HADITHI

HAKUNA aliyeamini alichokisikia, wala aliyeamini macho yake kwa kile alichokiona. Awali kulikuwa na vigelegele, ngoma, bashasha na furaha tele kwa watu wote waliohudhuria harusi hiyo. Bwana harusi Jerry Mohamed aliliongoza kundi la ndugu, rafiki na jamaa kutoka Dar es Salaam kwenda Kibaha kwa Mathias mkoani Pwani kwa ajili ya kufunga ndoa na mwanamke Vayajo waliyekubaliana kuoana. Mabasi, magari, bajaji, bodaboda, vyote vilimiminika kwenda huko kila mmoja akiwa na furaha tele. Kilichotokea ndicho kilicholeta mkasa mzima kwenye sakata hili la aina yake. Nini kimetokea? Kwa nini? Sababu ni nini? Na baada ya hapo nini kinaendelea? Kila nakala yako ya Nipashe itakupa majibu ya kisa hiki cha kushangaza.

# Harusi Imevunjika-17

Na Adam Fungamwangwo
(0716 350534)




HIVI wewe Vajayo una wazimu? Kumbe siku zote hizi unampiga na kunyanyasa mdogo wako kwa sababu ya Jerry? Wewe si ulimkimbia? Unadhani hadi leo tunaye hapa anakuja kwa sababu ya nani? Babu yako ni rafiki yake sana na ndiye akamshawishi kuja kumwona Zulfa, alipokuja hapa kwa hali aliyokuwa nayo, ikabidi amchukue na kumtibia, akakaa kwake hadi akapona, hadi unamuona hivi alivyo. Wewe hukuwepo na hadi leo hutaki kutuambia ulikuwa wapi. Ulisikia sisi tumekuuliza? Kaa na siri yako. Wewe hukuwepo, hukumuona Zulfa alivyokuwa, tumshukuru kijana yule. Umemfanyia mambo ya kifedhuli, lakini hakurudisha ubaya kwetu. Wewe unataka kumfanya aanze kutuona wabaya." akalalama mama Vayajo.

"Mwambie mwanao, asimfuatefuate mwanamume wangu."

"Wapi mama, umeshachelewa. Yaani umkimbie, hadi leo hajui alipokwenda, halafu kirahisirahisi tu hivi akurudie mfunge ndoa. Labda mkafunge huko, siyo hapa. Yaani nialike tena watu. Nitawafuata na uso gani? huu huu?" Mama alizidi kumpasha binti yake. Maneno hayo yalizidi kumnyong'nyesha Vayajo. Lakini alikuwa na lengo moja tu, kwenda kwa mganga wa kienyeji kama alivyoshauriwa na shoga yake Naa.

"Mama mwambie kabisa mwanao, siku akinipiga tena, au kuninyanyasa na habari zake za Jerry, mimi naondoka hapa. Naenda kwa huyo huyo Jerry. Nasingiziwa mwisho nimechoka. Mbona mimi nilishaambiwa nikaishi naye na wakubwa hapa. Walisema sisi mila za kabila letu zinaruhusu. Dada alivyotoroka mdogo wake anaweza kuchukua nafasi yake? Na aliitwa hadi hapa Lakini mimi nilikataa mbele yake. Leo hii naambiwa ni mpenzi wangu. Sasa ukizidi nitafanya kweli. Kwani si amenitibia, nimepona kwa ajili yake. Nimekaa kwake amenitunza kama malkia. Ana huruma, anajali, kwa nini..."

"Mama unamsikia?" Maneno hayo yalionekana kuwa kama moto kwenye moyo wa Vayajo. Tayari alikuwa anatetemeka kwa hasira. Alikuwa tayari kumvamia mdogo wake. Mama yao alikuwa katikati yao. Na alikuwa anamtazama jicho kali Vayajo. Na ndilo lililomfanya kusita kufanya chochote.

"Hebu nitokeeni hapa, ninyi watoto mna laana? Kwani hapa kwenye hiki kijiji ndio nimezaa peke yangu? Alaa... Nione mmoja wenu kampiga mwenzake, ndiyo mtanijua mimi nani." Mama akawapiga mkwara.

**"Mama mwambie kabisa mwanao, siku akinipiga tena, au kuninyanyasa na habari zake za Jerry, mimi naondoka hapa. Naenda kwa huyo huyo Jerry.**

****************************

"Nateseka mimi huku, sina raha. Kila siku dada yangu maneno, nimechoka mimi."

"Tatizo ni nini Zulfa?"

"Si huyu mchumba wako Vayajo. Yaani mimi ile kukaa kwako miezi mitatu kwa ajili ya kujiuguza na kujitazamia baada ya kutoka Hospitalini ndiyo imekuwa nongwa?"

"Nongwa ya vipi?"

"Eti mimi ni mpenzi wako, miezi mitatu niliyokaa, haikuwa bure."

"Amerudi hapo nyumbani?"

"Yupo, amerudi na mimi ndiyo imekuwa kama hasira zote anazitolea kwangu."

"Lakini dada yako si alinikimbia. Tena siku ya sherehe ya harusi? Mtu wa aina hiyo kweli anakupenda huyo?"

"Sijui sasa, lakini kanijia juu kuwa mimi utafikiri ndiyo niliyomshawishi akukimbie. Ananiambia nimemchukulia mchumba wake, na ana mpango wa kutaka kurudiana na wewe, lakini kikwazo ni mimi. Hivyo niachane na wewe."

"Ana wazimu huyo dada yako."

Ni mazungumzo kwa njia ya simu yaliyokuwa yakiendelea kati ya Jerry na Zulfa. Aliamua kumpigia simu shemeji yake ili amwambie kinachoendelea kwenye kijiji chao cha Msangani.

"Anasemaje huyo, anataka nini?"

"Anataka eti akutane na wewe, ili mzungumze, kwa sababu ilibaki ndoa tu peke yake, basi mfunge, hata haitakuwa na mtu yoyote, peke yenu tu." Zulfa alipomaliza kusema hivyo alisikia kicheko cha dharau kilichochanganyikana na hasira.

"Tena akushukuru wewe na babu. Ninyi ndio mlionifanya nirejee tena Msangani, vinginevyo angekuwa ananisikia kwenye bomba."

"Basi ninachofanyiwa huku, mimi napigwa, nafuatwa hadi kisimani, maji yanamwagwa, yaani kila siku visa tu, matusi ndiyo usiseme, yameshanichosha. Nafikiria kurudi zangu Morogoro kwa shangazi nikapumzike."

"Mmmh, Zulfa nikwambie kitu?"

"Enhee, sema Shem."

"Usifanye hivyo. Usiende Morogoro. Mimi wiki ijayo nitakuja huko ili kuliweka sawa hili suala."

"Utaliwekaje, wakati watu hawana amani huku? Labda amani ipatikane uje kumchukua Da' Vayajo." Jerry aliangua tena kicheko. Lakini haikuwa halisi.

"Sahau kuhusu hilo. Haiwezekani na haitowezekana. Mimi si mjinga kiasi hicho. Mtu akufanyie vile mbele ya watu wote unaowaheshimu na wanaokuheshimu, halafu tena umuweke ndani kwako. Wote waliokuwa kwenye harusi siku hiyo wakija kukutembelea nyumbani kwako wamkute, liwe simulizi mitaani?"

"Sawa, ila usimwambie kama nimekupigia simu tumeongea."

"Kwanza mimi nina muda naye? Sijawahi kuongea naye hata siku moja tangu alipoondoka. Kuna siku kama mbili tatu hivi tena hizi hizi za karibuni alikuwa ananipigia visimu vyake, mimi nikiona ni yeye sipokei na akatuma meseji sijajibu.

Hajatuma tena."

"Sawa Shem, maana..."

"Zulfa usiwe na wasiwasi, nitakachokuja kufanya huko na kuamua, hatokugusa au kukuuliza kitu tena kuhusu mimi."

Majibu hayo yalionekana kumfurahisha na kumfariji Zulfa. Hakujua ni nini hasa Jerry atakuja kusema, lakini alikuwa na uhakika kuwa suala la Jerry kumrudia tena dada yake halipo. Hilo ndilo lilimfurahisha zaidi. Hata yeye mwenyewe hakujua ni kwa nini.

Kutokana na furaha iliyomjaa moyoni akaazimia kuwa hatomjibu chochote dada yake. Atakaa kimya kama mjinga, akimsubiri Jerry aamue atakachoamua.

ITAENDELEA JUMAPILI



# KAKIRI KUWA MWENZA

MWANAMUZIKI nyota wa Bongo Fleva, Diamond Platnumz, amemtambulisha rasmi mwimbaji katika lebo ya WCB, Zuchu, kama mpenzi wake mbele ya familia yake.

Tukio hilo lilitokea majuzi wakati wote wawili walipohudhuria sherehe ya kutimiza miaka 37, ya dada yake Esma, ambayo ilihudhuriwa na wanafamilia, marafiki na watu wa karibu. Diamond alipopanda jukwaani kwa ajili ya kuelezea maisha ya dada yake, alimwita Zuchu kupanda jukwaani kwa kumtaja kama mwenzake.

"Sasa mwenzangu Zuhura akasema angependa sana tuje pamoja. Sasa mimi ni shabiki wa maagizo naomba aje awasilishe," alisikika Diamond akiwaambia watu.

Katika kuonyesha kwamba kumwita jina hilo hakukosea, Diamond alimtaja Zuchu kama wifi wa Esma pale walipokuwa wakishuka jukwaani kwenda kukaa katika nafasi walizopangiwa.

"Hapo ndipo tutajua kama ana mapenzi na wifi yake," alisema na kusababisha ukumbi kulipuka kwa furaha.

Esma alionekana kuwa na furaha zaidi baada ya Zuchu kunyanyuka na kwenda kumfuata jukwaani na kusimama karibu yake.

Kumekuwepo na minong'ono ya muda mrefu kuwa wawili hao wana uhusiano wa kimapenzi, licha ya wao wenyewe kukanusha uvumi huo.



# Q Chief aiweka 'The last Meal' ubaoni

MASHABIKI wa Muziki wa kizazi kipya, wanasubiri kwa hamu kusikia ngoma zinazobeba Albam mpya ya mwanamuziki mkongwe, Q Chief, ambayo tayari ametambulisha jina na idadi ya nyimbo.

Kupitia ukurasa wake wa Instagram, Q Chief ameitambulisha Albam hiyo kwa jina la 'The Last Meal', ambayo ndani yake kuna nyimbo hizo ambazo hakueleza kama kuna baadhi amefanya na wasanii wengine.

Msanii huyo amekuwa katika mchakato wa kunyanyuka tena baada ya muda mrefu kuwa katika mapitio magumu ya kupandisha umaarufu wake wa miaka iliyopita.



## ZISIKUPITE

### OSIMHEM KUIKAMUA UNITED

KLABU za Manchester United na Paris St-Germain zinapaswa kulipa ada ya uhamisho ya angalau pauni milioni 90 ikiwa zinataka kumsajili mshambuliaji mahiri wa Napoli na Nigeria, Victor Osimhen, mwenye umri wa miaka 24, katika dirisha la msimu wa joto. ***(ESPN)***

### SAKA ATAJWA CITY

ARSENAL imeweka kipaumbele cha kukubaliana mkataba mpya na nyota wake, Bukayo Saka, mwenye umri wa miaka 21 na beki wa Timu ya Taifa ya Ufaransa, William Saliba (21), huku Manchester City ikimtaka winga huyo wa England. (***Sports)***

### CHELSEA YAMTIZAMA MOUNT

BAADA ya dirisha dogo la usajili kufungwa, Chelsea imeelekeza nguvu zake katika kuongeza mkataba wa Mason Mount, mwenye umri wa miaka 24. Mkataba wa sasa kiungo huyo wa kati wa England unamalizika msimu wa joto wa mwaka 2024. (***90min***)

### AUBAMEYANG ASIKITIKA KUACHWA

VYANZO vya karibu na mshambuliaji wa Gabon, Pierre-Emerick Aubameyang vinasema mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 33 ameshtushwa na amesikitishwa kuachwa nje ya kikosi cha Chelsea kitakachoshiriki Ligi ya Mabingwa Ulaya na anaamini klabu hiyo inataka kumwondoa. (***Telegraph)***

### UNITED, GERNACHO SAFI

KLABU ya Manchester United imekubali kuongeza mkataba wa miaka minne wa winga mwenye umri wa miaka 18, Alejandro Garnacho, ambaye amekuwa akifanya vizuri na kucheza timu za taifa za vijana za Argentina. (***AS***)

### GREENWIID AIGAWA UNITED

INADAIWA kumetokea mgawanyika kuhusu iwapo mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya England, Mason Greenwood, mwenye umri wa miaka 21 aruhusiwe kuendelea na soka lake katika klabu hiyo au la. ***(Guardian)***

### GREENWOON KWENDA CHINA

MASON Greenwood anatazamia kuhamia katika Ligi Kuu China ili kuanza tena soka lake ikiwa Manchester United itaamua kumfuta kazi mara tu watakapokamilisha mchakato wa uchunguzi wa ndani. (***Sun)***

### WEST HAM, EVERTON VITANI

KLABU za West Ham United na Everton zitalazimika kusubiri hadi msimu wa joto kumsajili winga wa Suriname, Sheraldo Becker baada ya Union Berlin kusita kumruhusu mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27 kuondoka Januari kwa sababu ya malengo yao ya kutaka kushiriki Ligi ya Mabingwa Ulaya. (***Caught Offside)***

### ARAUJO ASHINDWA KUHAMA

UHAMISHO wa beki wa kulia wa LA Galaxy, Julian Araujo, kwenda Barcelona umeshindikana baada ya Shirikisho la Soka la Kimataifa (FIFA) kuamua nyaraka za kukamilisha uhamisho wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21 ziliwasilishwa kwa kuchelewa mno. ***(ESPN***)

### UNITED YAMTAJA BOOTH

KIUNGO wa kati wa zamani wa Utrecht ya Marekani mwenye umri wa miaka 21, Taylor Booth anafuatiliwa na Kocha wa Manchester United, Erik ten Hag. (***Mail)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# KLOPP AFICHUA SIRI MO SALAH KUKWAMA

## ●●● Asisitiza bado ni mchezaji mwenye kiwango cha dunia ingawa...

**LIVERPOOL,** England

JURGEN Klopp hana shaka kuhusu ubora wa Mohamed Salah na anaamini mshambuliaji huyo anaweza kufanya majukumu muhimu katika kufanikisha Liverpool kupata "kitu maalum" msimu huu.

Jana Liverpool iliingia dimbani kucheza na Wolves ikiwa katika nafasi ya 10 kwenye msimamo wa Ligi Kuu England, pointi 10 nyuma ya Manchester United iliyo nafasi ya nne katika vita vya kuwania tiketi ya kushiriki Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Wekundu hao, ambao pia wametolewa katika mataji mawili ya nyumbani na wanakutana na Real Madrid kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, haijakiona kiwango bora cha Salah msimu huu.

Ingawa Salah ndiye mfungaji bora wa Liverpool kwenye ligi msimu huu, ametikisa nyavu mara saba pekee katika mechi 19.

Katika misimu yake mitano ya Ligi Kuu England wakicheza kwenye Uwanja wa Anfield, alifikisha mabao 118.

Haya yanajiri baada ya kipindi cha karibu ambapo Salah alitia saini mkataba mpya wa kubakia hapo Liverpool huku mchezaji mwenzake, Sadio Mane akiruhusiwa kuondoka.

Lakini Klopp alimtetea nyota wake huyo kabla ya mechi ya Wolves, akiwaambia waandishi wa habari: "Mtazamo huo na mambo kama haya sio shida ya Mo.

"Mo ni mwanamichezo wa kiwango cha dunia, hivyo ndiye wa kwanza kuingia, wa mwisho, anafanya mazoezi makali. Sasa hafungi, lakini kuna watu wanafikiri kwanini walimpa mkataba?.

"Unaweza kuhoji tabia, maarifa, uwezo, kila kitu. Una haki ya kufanya kila kitu, lakini huwezi kufunga idadi ya mabao ambayo Mo alifunga kama wewe si mchezaji bora wa soka duniani."

Aliongeza: "Kuna wakati ambapo Mo bila shaka angefunga mwaka jana. Unafikiri hilo lilikuwa na uhusiano na mkataba mpya au chochote kile?

"Hiyo sio sawa. Mambo ni kama yalivyo na njia pekee tunaweza kuzuia maswali haya yote na mijadala ni kwa kufanya kiwango chetu cha juu, cha juu na ndicho tunachopaswa kufanya na kile ambacho tutakifanyia kazi.

"Tupo kwenye hilo, na bado tuko sawa, tuna matumaini, tunataka kucheza kwenye michezo na tunaamini katika nafasi zetu za kufikia kitu maalum hata mwaka huu."

SportPesa | LIVE IN PLA

MECHI KALI
TOTTENHAM
VERSUS
MANCHESTER CITY
1 | 4.00
X | 3.75
2 | 1.77

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# CITY SASA WAJIPANGA KUMNASA MAC ALLISTER




**MANCHESTER,** England

KLABU ya Manchester City imeripotiwa kumtambua kiungo wa kati wa Brighton and Hove Albion, Alexis Mac Allister kama mbadala wa Ilkay Gundogan mwishoni mwa msimu huu.

Mac Allister mwenye umri wa miaka 24 anafurahia msimu bora zaidi wa kikazi, huku tayari ana mabao matano katika mechi 17 alizocheza za Ligi Kuu England.

Kiungo huyo mbunifu pia aliichezea Argentina mechi sita wakati wa safari yao ya kutwaa ubingwa wa Kombe la Dunia nchini Qatar, akifunga bao lake la kwanza la kimataifa katika ushindi wa magoli 2-0 dhidi ya Poland katika hatua ya makundi.

Kuibuka kwake kama mchezaji mwenye uwezo wa kung'aa kwenye dunia, pamoja na mchango wake katika msimu wa hali ya juu wa Brighton, kumevutia macho ya Kocha wa City, Pep Guardiola.

Kwa mujibu wa Fichajes, Gundogan anatarajiwa kuondoka City mkataba wake utakapomalizika mwishoni mwa msimu huu, na Bernardo Silva anaweza kufuata ikiwa atapata matakwa yake na uhamisho wa kwenda LaLiga.

Fichajes imedai Brighton wameweka bei inayotakiwa kati ya pauni milioni 40, ikionyesha wako tayari kuachana naye kuliko Moises Caicedo (21), huku mikataba yao yote miwili ikimalizika ifikapo mwaka 2025.

# Aubameyang aondolewa kikosini



**LONDON,** England

PIERRE-Emerick Aubameyang ameondolewa kwenye kikosi cha Chelsea cha Ligi ya Mabingwa Ulaya, huku Kocha Mkuu, Graham Potter akiwaingiza wachezaji wapya Joao Felix, Enzo Fernandez na Mykhailo Mudryk.

Hatua hiyo ya kushangaza ya kumkata Aubameyang inaonyesha kushuka kwa kiwango cha mshambuliaji huyo akiwa na The Blues, ambaye alianza mchezo mara ya mwisho Novemba, mwaka jana.

Potter alionya Alhamisi kutakuwa na mazungumzo "ya kutatanisha" mbeleni alipokuwa akihitimisha kundi lake kwa muda uliosalia wa msimu wa Chelsea ya Ulaya, na kumwacha Aubameyang (33).

Mchezaji huyo wa zamani wa Arsenal na Barcelona amefunga mabao matatu pekee msimu huu katika mechi 18, kati ya hizo 10 ameanza.

Aubameyang alianza katika mechi zote sita za makundi za Ligi ya Mabingwa Ulaya akifunga nyumbani na ugenini dhidi ya AC Milan.

Potter badala yake ameweka imani yake kwa Kai Havertz, ambaye ametumia muda mwingi wa maisha yake kama kiungo mkabaji, pamoja na washambuliaji Joao Felix, ambaye yuko kwa mkopo kutoka Atletico Madrid, na Mudryk, aliyewasili kutoka Shakhtar Donetsk.

CHEZA USHINDE KASINO

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SPORTPESA APP

PAKUA APP YETU, BET LEO UWE MILIONEA

MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMAPILI - 05/02/2023

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:15 | 5287 | Cambuur vs Ajax | 9.93 | 5.76 | 1.24 |
| 14:30 | 4850 | Spezia vs Napoli | 7.92 | 4.85 | 1.34 |
| 15:00 | 1316 | St Johnstone vs Celtic | 10.92 | 6.35 | 1.21 |
| 15:00 | 5907 | Clermont Foot vs Monaco | 3.89 | 3.64 | 1.84 |
| 15:30 | 5517 | Royal Antwerp vs Brugge | 2.49 | 3.39 | 2.65 |
| 15:45 | 5777 | El Daklyeh vs Aswan | 2.75 | 2.90 | 2.80 |
| 16:00 | 1206 | Hatayspor vs Kasimpasa | 2.38 | 3.44 | 2.75 |
| 16:00 | 3110 | Mallorca vs Real Madrid | 4.90 | 3.55 | 1.71 |
| 16:15 | 1818 | FC Sion vs FC Zurich | 2.70 | 3.34 | 2.47 |
| 16:30 | 1440 | GO Ahead Eagles vs NEC Nijmegen | 2.42 | 3.33 | 2.73 |
| 16:30 | 4667 | Feyenoord vs PSV Eindhoven | 2.14 | 3.47 | 3.08 |
| 16:30 | 4864 | TS Galaxy FC vs Kaizer Chiefs | 2.86 | 2.91 | 2.58 |
| 17:00 | 2305 | Lorient vs Angers | 1.86 | 3.49 | 3.98 |
| 17:00 | 3853 | Strasbourg vs Montpellier | 2.09 | 3.19 | 3.53 |
| 17:00 | 4620 | AC Ajaccio vs Nantes | 2.68 | 3.03 | 2.68 |
| 17:00 | 4642 | Nottingham vs Leeds | 2.54 | 3.24 | 2.64 |
| 17:00 | 4938 | Torino vs Udinese | 2.27 | 3.13 | 3.13 |
| 17:00 | 5013 | AJ Auxerre vs Reims | 3.34 | 3.34 | 2.10 |
| 17:30 | 4568 | Stuttgart vs Werder Bremen | 2.02 | 3.52 | 3.32 |
| 18:00 | 5107 | Mechelen vs Charleroi | 2.22 | 3.44 | 2.99 |
| 18:00 | 5466 | Panathinaikos vs Lamia | 1.37 | 4.15 | 9.57 |
| 18:15 | 4694 | Girona vs Valencia | 2.20 | 3.20 | 3.30 |
| 18:15 | 5467 | Parma vs Genoa | 2.57 | 3.06 | 2.74 |
| 18:30 | 1376 | GD Chaves vs Maritimo | 2.06 | 3.23 | 3.58 |
| 18:30 | 1431 | FC Luzern vs BSC Young Boys | 3.29 | 3.55 | 2.05 |
| 18:30 | 2193 | Atromitos vs AEK Athens | 6.57 | 4.03 | 1.48 |
| 18:30 | 4421 | Sporting Braga vs Famalicao | 1.37 | 4.77 | 7.35 |
| 18:30 | 5511 | FC Winterthur vs FC Lugano | 3.18 | 3.45 | 2.12 |
| 18:45 | 3209 | Groningen vs Twente | 4.97 | 3.83 | 1.62 |
| 19:00 | 1027 | Al-Shamal vs Al-Sailiya SC | 2.35 | 3.37 | 2.65 |
| 19:00 | 5819 | Galatasaray vs Trabzonspor | 1.67 | 3.81 | 4.66 |
| 19:05 | 3312 | Brest vs Lens | 4.28 | 3.58 | 1.78 |
| 19:30 | 3582 | Tottenham vs Manchester City | 4.00 | 3.75 | 1.77 |
| 19:30 | 5056 | VfL Wolfsburg vs Bayern Munchen | 4.74 | 4.45 | 1.55 |
| 19:30 | 5170 | Hajduk Split vs HNK Rijeka | 1.48 | 3.98 | 5.79 |
| 20:00 | 1163 | Sparta Prague vs Mlada Boleslav | 1.53 | 4.26 | 5.82 |
| 20:00 | 2999 | El Ittihad Alexandria vs Ismaily SC | 2.04 | 3.00 | 3.99 |
| 20:00 | 4853 | Ceramica Cleopatra vs Enppi Club | 1.86 | 3.24 | 4.39 |
| 20:00 | 5154 | Fiorentina vs Bologna | 1.81 | 3.42 | 4.27 |
| 20:30 | 2823 | KAA Gent vs Racing Genk | 2.29 | 3.43 | 2.89 |
| 20:30 | 2922 | Real Sociedad vs Valladolid | 1.43 | 4.29 | 7.38 |
| 21:00 | 2443 | Panetolikos vs Asteras Tripolis | 2.57 | 2.97 | 2.87 |
| 21:00 | 3517 | Porto vs FC Vizela | 1.19 | 6.35 | 12.90 |
| 21:15 | 1632 | Union Saint Gilloise vs Zulte Waregem | 1.36 | 4.97 | 7.16 |
| 21:30 | 4760 | PAOK vs Olympiakos | 2.42 | 3.08 | 2.97 |
| 22:00 | 2563 | CFR Cluj vs Steaua Bucuresti | 2.25 | 3.12 | 3.17 |
| 22:45 | 1845 | Inter vs AC Milan | 1.93 | 3.42 | 3.71 |
| 22:45 | 5626 | Marseille vs Nice | 1.68 | 3.74 | 4.68 |
| 23:00 | 3132 | Barcelona vs Sevilla FC | 1.38 | 4.61 | 7.94 |
| 23:30 | 2288 | Gil Vicente vs FC Arouca | 2.24 | 3.18 | 3.18 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# CHIPUKIZI YATAMBA KUTWAA UBINGWA LIGI KUU ZANZIBAR

**Na Hawa Abdallah,**
ZANZIBAR

KOCHA Msaidizi wa Chipukizi FC, Mzee Ali Abdallah, amesema kikosi chake kiko imara na ni kati ya timu zilizojitosa katika mbio za kuwania ubingwa wa Ligi Kuu Zanzibar msimu huu.

Akizungumza na gazeti hili jana, Abdallah alisema ingawa ni mapema kusema nani atashinda taji hilo, lakini ana imani kubwa ya kutwaa taji hilo msimu huu kutokana na mwenendo wa matokeo mazuri wanayoyapata.

Abdallah alisema msimu huu umekuwa mzuri kwa upande wao kuanzia katika mechi za mzunguko wa kwanza hadi hatua ya lala salama ilipoingia na wamejipanga kuendelea kufanya vizuri ili watimize malengo yao.

"Tumeanza vizuri kuanzia mzunguko wa kwanza hadi hatua hii ya lala salama, pia tumeanza vizuri japo tumecheza michezo michache," alisema Abdallah.

Aliongeza mafanikio waliyoyapata katika msimu huu yametokana na kuwapo kwa udhamini ambao umesaidia kwa kiasi kikubwa timu kupata fedha za uendeshaji na kufanya usajili wa wachezaji wenye uwezo ambao wameongeza ushindani.

"Lakini bado tunaiomba ZFF iendelee na jitihada za kusaka wadhamini wengine ili wasaidie kuboresha Ligi Kuu Zanzibar, kwa kufanya hivyo watazidisha ushindani," alisema kiongozi huyo.

Aliongeza kila timu inahitaji kumaliza msimu ikiwa na matokeo bora kwa sababu ya kujihakikishia kuondoka na zawadi ambazo zinatolewa na wadhamini hao.

"Tunazidi kujipanga katika kila mchezo tunaocheza, tunajua hakuna mechi rahisi, kila mchezo ni sawa na fainali, lakini msimu huu tumejipanga kuhakikisha tunatwaa ubingwa," alisema Abdallah.

Chipukizi FC yenye makazi yake Kisiwani Pemba ambapo ipo katika nafasi ya sita kwenye msimamo wa Ligi Kuu Zanzibar ikiwa na pointi 29.



Wanafunzi wa darasa la kwanza wa Shule ya Msingi Al- Hikma wakiimba katika hafla ya kuwapongeza wanafunzi waliomaliza kidato cha nne mwaka jana katika shule hiyo na kufanya vizuri. Shule hiyo imeshika nafasi ya pili katika shule za Kiislamu nchini. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## *Yanga yaiwaza robo fainali CAF*

INATOKA UK 24

Nabi alisema wapinzani wao wana kikosi imara kutokana na kuwa na uwezo wa kulazimisha mashambulizi.

"Ni kweli tumewafatilia wapinzani wetu na kuona ubora wao ikiwemo safu yao ya ushambuliaji na ulinzi, tunahitaji kujiimarisha na kufanyia kazi mapungufu yetu ili kupata matokeo mazuri, " alisema Nabi.

Yanga wataanza kushuka ugenini Jumapili kuwavaa US Monastir na baadaye itarejea nyumbani kuikaribisha TP Mazembe katika mchezo utakaofanyika Febuari 19, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

## Robertinho asema Simba 'levo' mpya

INATOKA UK 24

huo yameongoza molari ya wachezaji kuelekea mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Horoya AC ya Guinea ambayo watacheza ugenini.

Naye Kocha Mkuu wa Singida Big Stars, Hans van Pluijm, alisema wachezaji wake walipambana lakini Simba walistahili kupata ushindi kwa sababu ya ubora wa timu hiyo.

Pluijm alisema walitengeneza nafasi za wazi lakini wachezaji wake walishindwa kuzitumia vyema huku wakifanya makosa ambayo Simba iliyatumia vizuri na kupata ushindi katika mechi hiyo.

"Tulizidiwa na Simba walistahili ushindi kwa kuwa walikuwa bora, wachezaji walipambana kutafuta matokeo, walikuwa makini na nafasi walizitengeza, tumeona madhaifu yetu na tunaenda kuyafanyia kazi ili kujiandaa na mchezo ujao," alisema Pluijm.

Ili kuendelea kujiimarisha, Simba jana usiku ilitarajia kuikaribisha Al Hilal kutoka Sudan katika mechi ya kirafiki ya kimataifa. Al Hilal inajiandaa kwenda kuwakabili Mamelodi Sundowns, katika mchezo wa Ligi ya Mabingwa Afrika.

# Michezo

Nipashe

Jumapili Februari 5, 2023






Klopp afichua siri Mo Salah kukwama




Kiungo wa Simba, Clatous Chama (kulia), akijiandaa kumtoka beki wa Singida Big Stars FC, Biemes Carno, katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam juzi usiku. Simba ilishinda mabao 3-1. **PICHA: SIMBA SC**

## Robertinho asema Simba 'levo' mpya

**Na Saada Akida**

BAADA ya kuvuna pointi tatu katika mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Singida Big Stars, Kocha Mkuu wa Simba, Roberto Oliviera 'Robertinho', amewasifu wachezaji kwa kupambana na kuibuka na ushindi wa mabao 3-1.

Mabao ya Simba katika mechi hiyo yalifungwa na Jean Baleke dakika ya nane, Saido Ntibazonkiza dakika ya 20 na Pape Osmane Sakho dakika 63 huku lile la kufutia machozi la Singida Big Stars likipachikwa na Bruno Gomes dakika ya 34.

Robertinho alisema wachezaji wake walicheza vizuri katika mechi hiyo kuanzia kwenye safu ya ulinzi, kiungo na ushambuliaji, jambo ambalo ni zuri kama kocha anajivunia.

Alisema anafurahi timu yake imeanza kucheza vizuri kwa kufuata falsafa zake akiwa na muda mfupi tangu alipokabidhiwa kikosi hicho.

"Niwapongeze wachezaji wangu kwa kupambana na kucheza katika kiwango bora zaidi, nimeona ubora wa nyota wangu, nafurahi hata wale wapya wameanza kuingia katika mfumo wangu. Pia niwapongeze zaidi wapinzani wetu walikuwa bora na kuufanya mchezo kuwa wa ushindani mkubwa," alisema Robertinho.

Aliongeza matokeo ya mchezo

INAENDELEA UK 23

# *Yanga yaiwaza robo fainali CAF*

### Yajipanga kuvuna pointi sita huku ikitamba Watunisia hawachomoki...

**Adam Fungamwango na Saada Akida**

KATIKA kuhakikisha inajiweka kwenye nafasi nzuri ya kutinga robo fainali ya michuano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika, vinara wa Ligi Kuu Bara, Yanga imesema inahitaji kupata ushindi kwenye mechi zake mbili za kwanza za hatua ya makundi, imeelezwa.

Akizungumza na gazeti hili jana, Ofisa Habari wa Yanga, Ali Kamwe, alisema timu yao imedhamiria kuvuna pointi sita katika mechi za awali kwa kuanza na kushinda mchezo wa ugenini Tunisia dhidi ya Monastir kama walivyofanya walipoifuata Club Africain ya nchini humo.

Kamwe alisema malengo yao pia ni kupambana na kushinda mechi inayofuata itakayochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa dhidi ya TP Mazembe kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC).

"Tutaanzia ugenini dhidi ya Monastir Februari 12, tunataka mechi hiyo tukapate tena ushindi kama tulivyofanya dhidi ya Club Africain, kama vilevile wanachama na mashabiki wetu walivyotuombea kwenye mechi ile tulivyokuwa Tunisia, basi safari hii wazidishe maombi ili tuweze kushinda tena tupate pointi tatu, halafu tutarudi kucheza nyumbani na TP Mazembe," alisema Kamwe.

> **Ofisa huyo amewaomba wana chama na mashabiki wa timu hiyo kujitokeza kwa wingi katika mechi zote za nyumbani ili kuongeza chachu na hamasa kwa wachezaji wao.**

"Hili la kusaka pointi sita za mwanzo asiachiwe Nabi (Nasreddine) au Mayele (Fiston) peke yake, bali ni jukumu la wote, wanachama na mashabiki, tukipata pointi sita hizi, zitakuwa zimetuweka kwenye mazingira mazuri ya kusonga mbele," Kamwe alisema.

Aliongeza Yanga imekuwa haifanyi vizuri katika mechi zinazochezwa nyumbani jambo ambalo hawataki kuliona msimu huu linaendelea.

"Sisi Yanga tumekuwa hatufanyi vizuri hasa kwenye mechi za nyumbani, lakini kila jambo ni lazima lifike mwisho, kwa hiyo sasa ni lazima tushinde na tukifanya hivyo tutakuwa kwenye nafasi nzuri sana ya kufuzu kwenye hili kundi," aliongeza bosi huyo.

Alitamba msimu huu walifanya usajili mzuri na pia katika dirisha dogo waliongeza nguvu kwa kuwanasa, Kennedy Musonda aliyekuwa akigombea pia na TP Mazembe na Mamadou Doumbia.

Aliongeza maandalizi ya safari ya kuelekea Tunusia yamekamilika na msafara utaondoka nchini keshokutwa.

Alisema kwa sasa Yanga wakiwa Tunisia sio wageni tena kwa sababu walipata matokeo mazuri huko kwa kumtoa Club Africain, hivyo watatumia 'style' ile ile iliyowavusha.

Naye Kocha Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi, aliliambia gazeti hili ameona safu ya ushambuliaji ya wapinzani wao, US Monastir na kuanza kujipanga kucheza kwa umakini na kuimarisha safu yake ya ulinzi.

INAENDELEA UK 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >